# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Jumanne Januari 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580465

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Rufani** ya kina Mdee bado ni kaa la moto

UKURASA 3



**Vifaa** barabara Morroco-Mwenge vyadaiwa kuibwa

UKURASA 4

# Ndizi za 2,000/- zilivyofanikisha wizi wa mtoto

UKURASA 2



## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**TMA YAHADHARISHA MVUA KUBWA KUNYESHA**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa...

UKURASA WA 15

**TAKUKURU KUSIKILIZA MADAI YA RUSHWA TANESCO**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)...


## JPM atoa siku saba wazabuni kulipwa

UKURASA 3



Mkazi wa Kitongoji cha Ipwasi katika Kijiji cha Nyamahana, Kata ya Mlowa, wilayani Iringa, mkoani Iringa, amejifungua watoto mapacha wa jinsi ya kike ambao wanatumia moyo mmoja. Mapacha hao waliopewa majina ya Dorice na Dorcas, walizaliwa katika Hospitali Teule ya Tosamaganga wilayani Iringa. Miaka 24 iliyopita mkoani humo walizaliwa mapacha Maria na Consolata walioungana sehemu ya kiuno, lakini walifariki dunia mwaka 2018. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu




# Wabunge machachari wapangwa kamati nyeti

UKURASA 2

**MICHEZO** STARS, ZAMBIA MECHI YA KIBABE LEO UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Ndizi za 2,000/- zilivyofanikisha wizi wa mtoto

**Na Thobias Mwanakatwe**

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia mwanamke muuza matunda, Severina Msongole (47), mkazi wa Kijiji cha Isangawana, Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuiba mtoto wa miezi minne.

Mwanamke huyo anayefahamika kama Neema, anadaiwa kufanikisha wizi wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa), baada ya kumlewesha kwa soda inayodaiwa kuwekwa dawa aina ya 'Piriton' mama mzazi wa mtoto huyo, Maria Msyaliha (19), akiwa anauza ndizi mnadani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, juzi alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa alikamatwa Januari 15 mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana, katika kijiji cha Isangawana, wilayani Chunya.


Kamanda Kyando, alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa la kuiba mtoto huyo Januari 7, mwaka huu, baada ya kununua ndizi mbivu za Sh. 2,000 na kutengeneza urafiki uliosababisha kufanikisha tukio hilo.

"Mama wa mtoto wakati amepanga ndizi zake kwa ajili ya kusubiri wateja, ghafla alijitokeza mwanamke (Neema) aliyekuja kama mteja akanunua ndizi za 2,000 na kutoa noti ya Sh. 5,000," alisema Kamanda Kyando na kuongeza:

"Wakati muuzaji akihangaika kupata chenji ghafla mtuhumiwa alimuomba waongozane hadi nyumba ya kulala wageni alikofikia jirani na mnadani hapo, ili akampatie fedha yake baada ya kukosa chenji na walipoingia chumbani alimpatia Sh. 2,000 na kumkaribisha soda."

Kamanda Kyando aliongeza kuwa baada ya kupata kinywaji walitoka nje huku mtuhumiwa akimwomba mama wa mtoto huyo amsindikize kituo cha mabasi kwa kumsaidia kubeba mizigo aliyokuwa nayo, na wakiwa njiani ghafla mzazi huyo alianza kujisikia kizunguzungu na kupoteza fahamu, hali iliyompa mwanya mtuhumiwa huyo kuondoka na mtoto.

Aidha, Kamanda Kyando (pichani) alisema baada ya mahohjiano, mtuhumiwa alikiri kufanya tukio hilo ili kumridhisha mumewe wa sasa ambaye amekuwa akimsumbua mara kwa mara, akitaka mtoto ambaye baada ya jitihada za kupata kushindikana kutokana na kuwa na matatizo ya ujauzito kuharibika mara kadhaa.



## TMA yatoa tahadhari mvua kubwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya mvua kubwa itakayoambatana na madhara mbalimbali katika mikoa 12 nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, mvua hiyo itaanza kunyesha kesho katika mikoa ya Ruvuma, kusini mwa mkoa wa Morogoro, Lindi na Mtwara.

Aidha, Januari 21 hadi 22, mwaka huu, mvua pia zitaendelea katika mikoa hiyo ikiwamo Njombe na Pwani.

"Athari zitakazojitokeza ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji pamoja na ucheleweshaji wa baadhi ya shughuli za usafirishaji," ilisema.

Aidha, TMA imewataka wananchi kujiandaa na kuchukua tahadhari mapema.

# Wabunge machachari wapangwa kamati nyeti

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amefanya uteuzi wa wajumbe wa kamati mbalimbali za bunge, huku wabunge machachari wakipangiwa kamati nyeti.

Pia wabunge wengine wakiwamo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA) wamepangiwa kamati zaidi ya moja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ofisi ya Bunge jana, Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imelipa Bunge uhalali wa kuunda kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake.

Aidha, Spika huyo alifanya uteuzi huo kwa mujibu wa Kanuni ya 135(3) na kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika kanuni 135(5), baada ya uteuzi huo, wajumbe hao wanawajibika kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 135(10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Wabunge hao ni pamoja na Askofu Josephat Gwajima ambaye amepangiwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Pia aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei, amepangiwa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Eric Shigongo pia amepangiwa kamati hiyo, Alexander Mnyeti, ameteuliwa kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Wengine ni Humphrey Polepole ambaye ameteuliwa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Salome Makamba ameteuliwa kamati ya bunge ya Kanuni za Bunge na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Esther Bulaya ameteuliwa katika kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Masuala ya Ukimwi.

January Makamba, Livingstone Lusinde na Christopher Ole Sendeka wamepangiwa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Jesca Kishoa, Joseph Musukuma wamepangiwa kamati ya Nishati na Madini huku Esther Matiko, Halima Mdee na Mrisho Gambo wakipangiwa kamati ya Bajeti.

Ridhiwani Kikwete ameteuliwa katika kamati mbili ambazo ni ya Sheria Ndogo na Kamati ya Kanuni za Bunge, huku Japhet Hasunga aliyekuwa Waziri wa Kilimo akiteuliwa kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Naghenjwa Kaboyoka ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya PAC kwenye Bunge lililopita, ameteuliwa kwenye kamati hiyo na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge huku Aida Khenani akiteuliwa kamati ya PAC na Kamati ya Kanuni za Bunge.

Aiyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla na Anathropia Theonest wamepangiwa kamati ya PAC.

Katika kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), wameteuliwa Grace Tendega, Conchesta Rwamlaza na Nape Nnauye.

**WENYEVITI WA KAMATI**

Waliopeta nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwenye kamati mbalimbali ni pamoja Selemani Kakoso na Anne Kilango Malecela (Kamati ya Miundombinu), Stanslaus Nyongo na Aloyce Kamamba Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii).

Katika kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Mwakiposa, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya LAAC amechaguliwa Grace Tendega na Selemani Zedi.

Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Mwenyekiti ni Dk. Christine Ishengoma na Makamu wake ni Athuman Maige.

Aidha, Polepole ambaye ni Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi ya CCM, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na Makamu wake ni Abdallah Chaurembo.

Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii amechaguliwa Mwenyekiti Aloyce Kwezi na Makamu wake ni Dk. Pius Chaya.

Kamati ya Nishati na Madini amerudi kwenye nafasi yake Dastan Kitandula huku Makamu wake akiwa Seif Gulamali.

Kamati ya PAC amerudishwa tena kushika wadhifa huo Naghenjwa Kaboyoka na Makamu wake ni Japhet Hasunga.

Kwa upande wa Kamati ya Katiba na Sheria, aliyechaguliwa kuwa mwenyekiti ni Mohamed Mchengelwa.

Makamu wa Kamati ya Katiba na Sheria ni Najma Murtaza Giga ambaye amerudi kwenye nafasi hiyo, huku Kamati ya PIC, Mwenyekiti wake ni Atupele Mwakibete na George Malima.

Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni Mussa Zungu na Vincent Mbogo, huku Kamati ya Masuala ya Ukimwi ni Fatma Toufiq na Dk.Alice Kaijage.

Kamati ya Bajeti Mwenyekiti wake ni Sillo Baran, huku Makamu Mwenyekiti ni Omary Kigua na katika kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge amerudi kwenye nafasi yake Emmanuel Mwakasaka huku Makamu Mwenyekiti akiwa ni Stella Ikupa.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | RESPIQUIS C. MUTTA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - KITUNDA | UMOJA PROFESSIONALS | 19-02-2021 |
| 2 | CHRISTOPHER N. ATHUMANI | GARI | TOYOTA RAV 4 T 237 CYL | UMOJA PROFESSIONALS | 25-01-2021 |
| 3 | ULM INVESTMENT | NYUMBA | HATI – YOMBO VITUKA | J & J RECOVARIES | 12-02-2021 |
| 4 | CHRISTOPHER N. ATHUMANI | GARI | SUZUKI CARRY T 723 CTN | UMOJA PROFESSIONALS | 01-02-2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Taratibu na gharama za kubadili hati miliki kadi ya gari ni juu ya mnunuzi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika kikao kazi na Gavana wa Benki Kuu, Wakurugenzi wa Benki za NBC, NMB, CRDB, TPB, TADB, AZANIA, TIB pamoja Mifuko ya NSSF na PSSSF kwenye ukumbi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mlimwa jijini Dodoma, jana. Kikao hicho pia kulihudhuriwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge na Waziri Mkuu), Tixon Nzunda. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# JPM atoa siku saba wazabuni kulipwa



**Na Restuta Damian,** BUKOBA

RAIS John Magufuli ametoa siku saba kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kuzilipa kampuni binafsi zilizosambaza vifaa vya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wavulana ya Ihungo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, iliyoathiriwa na tetemeko la ardhi mwaka 2016.

Shule ya Sekondari ya Ihungo imefanyiwa ukarabati kwa kujenga majengo mapya na machache kwa gharama ya Sh. bilioni 10.9 zikiwamo Sh. bilioni 6.1 zilizotolewa kwa ufadhili kutoka Serikali ya Uingereza na Sh. bilioni 4.8 zilizotolewa na Serikali ya Tanzania.

Ujenzi mpya umefanywa kwa majengo matatu ya ghorofa yenye jumla ya vyumba 24 vya madarasa, mabweni 3, vyoo na nyumba 30 za walimu na kwamba ukarabati mkubwa umefanyika kwenye maabara 3, karakana na mifumo ya maji, umeme na taka.

Akizungumza jana baada ya uwekaji jiwe la msingi katika Chuo cha Mamlaka ya Ufundi Stadi VETA), mkoani Kagera na uzinduzi wa majengo ya Shule ya Ihungo, Rais Magufuli alisema bado kuna malalamiko ya kutolipwa kampuni zilizosambaza vifaa vya ujenzi huo.

Alisema watu walikuwa wakitumia nguvu kazi zao kusambaza vifaa vya ujenzi wa majengo ya shule hiyo mpaka kufikia hatua ya kutumiwa ujumbe mfupi wa maandishi kwake kwamba hawajalipwa.

"Nilipata SMS kwamba wamefikia hatua ya kufilisika sijui wapo hapa, watu wanatumia nguvu kazi zao walipeni, wengine nimesikia walilipwa, natoa siku saba walipwe," aliagiza Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema shule hiyo imejengwa kwa ufadhili wa serikali ya Uingereza kwa gharama ya Sh. bilioni 6.1, huku serikali ya Tanzania ikitoa Sh. bilioni tano.

"Serikali ya Uingereza kwa kushirikiana na Tanzania imeweza kufanikisha kutoa kiasi cha Sh. bilioni sita na sisi tumetoa Sh. bilioni tano ambazo zimetumika kujenga shule hii," alisema Rais Magufuli.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alimshukuru Rais Magufuli kwa kutoa kipaumbele kikubwa katika masuala ya elimu ikiwamo maelekezo yake ya kujenga vyuo vya ufundi nchi nzima na kukarabati Shule ya Sekondari Ihungo baada ya kuathiriwa na tetemeko la ardhi, ambapo ukarabati uliofanywa umeongeza uwezo wa shule hiyo kutoka kupokea wanafunzi 640 hadi kufikia wanafunzi 1,152 kama alivyoelekeza.

Aidha, alibainisha kuwa katika miaka 5 iliyopita shule kongwe 84 kati ya 89 zimekarabatiwa ilhali 5 zilizobaki zikiendelea kukarabatiwa na kwamba imepanga kujenga shule ya sekondari ya wasichana yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa kila mkoa.

Kwa upande wa ujenzi wa Chuo cha VETA Kagera kinajengwa katika eneo Bulugo Mjini Bukoba kwa ufadhili wa Serikali ya Watu wa China kwa gharama ya Sh. bilioni 22, ujenzi wake umefikia asilimia 50.7 na kinatarajiwa kukamilika Agosti 2021 kikiwa na uwezo wa kuchukua kati ya wanafunzi 800 na 1,000.

Aliongeza kuwa chuo hicho kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi kati ya 800 hadi 1,000.

Alisema kwa sasa Tanzania ina vyuo vya VETA 712, kati ya hivyo serikali ina vyuo 62 kati ya hivyo 20 vipo ngazi ya mkoa na 42 ngazi ya wilaya.

Aliongeza kuwa serikali inatarajia kujenga vyuo vingine 33 vipya na kwamba kati ya hivyo, vinne vitakuwa ngazi ya mkoa na 26 ngazi ya wilaya na kwamba vitakapokamilika vitadahili wanafunzi 65, 640.

Aidha, Rais Magufuli amesema kujengwa kwa Chuo cha VETA Kagera ni sehemu ya juhudi za kuongeza vyuo vya VETA kwa Watanzania, ambapo vimeongezeka kutoka 672 (2015) hadi kufikia vyuo 712 (2020) na kwamba hivi sasa vyuo 33 vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi zaidi ya 60,000 vinaendelea kujengwa.

# Rufani ya kina Mdee bado ni kaa la moto

**Na Elizabeth Zaya**

HATIMA ya rufani ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) kina Mdee na wenzake 18 bado ni kaa la moto, baada ya uongozi wa chama hicho kusema bado haijulikani ni lini baraza hilo litaitishwa ili kuwajadili.

Kauli hiyo ya CHADEMA imekuja ikiwa tayari kamati za bunge zimeanza na vikao vya bunge vikitarajiwa kuanza mwanzoni mwa Februari.

Akizungumza na Nipashe jana, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, Benson Kigaila, alisema bado hawajapanga ni lini kikao hicho cha baraza kitaketi.

"Kwa mujibu wa Katiba ya chama chetu, kikao cha baraza kinatakiwa kikaliwe mara moja kwa mwaka, kwa hiyo ninachoweza kukuambia ni kwamba rufani hizo zitajadiliwa mpaka pale kikao kitakapokaliwa," alisema Kigaila.

"Na hakikaliwi kwa dharura isipokuwa kwa kufuata mipango na taratibu za chama. Ukisema kikao kikae kwa sababu ya dharura, kitafanyika mara ngapi, ijulikane kwamba kikao kitaketi lakini lini ni mpaka itakapopangwa."

Mdee na wenzake wamekata rufani ya kupinga kuvuliwa uanachama uliofanywa na Kamati Kuu ya CHADEMA Novemba mwaka jana, baada ya kwenda kuapa bungeni kama wabunge wa viti maalum.

Chama hicho kilitangaza kutotambua matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana na kutovitambua viti maalum ambavyo kilipata katika uchaguzi huo.

Akitoa hotuba yake mwanzoni mwa mwezi huu, Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema baada ya wabunge hao kukata rufani, wanaamini kwamba uongozi wa juu wa chama hicho baada ya kuketi kwa ajili ya kuamua hatima yao, utatenda haki kwa kila mtu.

"Chama chetu bila kuwahusisha viongozi wa chama na bila maamuzi ya chama, mama na dada zetu waliapishwa katika mazingira ya kutatanisha na bila kuidhinishwa na chama," alisema na kuendelea:

"Walikata rufani, vikao stahiki vya chama vitakaa wakati mwafaka na kusikiliza rufani zao, na nina hakika haki itatendeka."

DERM GROUP

DERM ELECTRICS (T) LIMITED

Derm Plaza 15th Floor, New Bagamoyo road, Plot 18, Block 45A, Kijitonyama, P.O Box 4756, Dar Es Salaam. Telephone: +255 22 2774507

PUBLIC NOTICE



**Derm Electrics (T) Ltd** is here to notify the public that;

**KELVIN KILIAN CHUMA**

Is no longer an employee of

**Derm Electrics (T) Ltd effective 13/01/2021**

Please take note that he is not allowed to perfom any transactions on behalf of the company.

**Derm Electrics (T) Ltd will not be held responsible for any transaction made by the above mentioned.**

Derm Elevators DTsmart

# Vifaa mradi barabara Morocco hadi Mwenge vyadaiwa kuibwa

**Na Mwandishi Wetu**

VIFAA vya mradi wa upanuzi wa barabara ya Morocco hadi Mwenge, jijini Dar es Salaam, vimedaiwa kuibwa na kukutwa katika kibanda cha chuma chakavu, imefahamika.

Wakati vifaa hivyo vikidaiwa kuibwa, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kinondoni, linamshikilia mfanyabiashara wa chuma chakavu, Shaban Athumani, kwa tuhuma za kuhusika na vizi wa vifaa hivyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MAC Contractors ambayo ni mbia wa ujenzi wa mradi huo, Solomon Kimaro, alisema jana kuwa wizi huo ulibainika juzi wakati mafundi wakiwa wanaanza kazi na kukuta baadhi ya vifaa vikiwamo lami na reki za kusambazia lami vikiwa havipo kwenye kambi ya ujenzi.

Hatua hiyo, alisema iliwafanya wafanyakazi katika eneo la mradi kuripoti kwa uongozi na hatimaye kutolewa taarifa polisi ambao kwa kushirikiana nao, walianza uchunguzi mara moja.

Alisema katika uchunguzi huo, polisi kutoka kituo kidogo cha Mwenge, walifika katika ofisi na kuanza kazi na katika upekuzi wao, walikuta baadhi ya vifaa vikiwa katika kibanda cha chuma chakavu kilicho karibu na ofisi za kampuni hiyo.

"Imetutia hofu kuona vifaa vya mradi mkubwa kama huu vikiibwa na watu kwa ajili ya kutengeneza chuma chakavu tena watuhumiwa wako karibu na ofisi za mradi huu. Huu ni uharibifu wa hali ya juu, tunaomba hatua zichukuliwe kukomesha tabia hii.

"Sasa kama vifaa kama reki na lami vinaibwa. Hii inamaanisha kwamba hata baadhi ya miundombinu inayofungwa katika mradi inatakiwa kuwe na ulinzi kwani watu wanaweza kuhujumu miundombinu baada ya kukamilika na kuwa hasara," alisema.

Naye Ofisa Usalama wa MAC Contractors, Lutengano Mwabwagila, alisema vifaa vilivyoibwa ni reki nne ambayo kila moja ina gharama ya Sh. 140,000 pamoja na lami yenye ujazo wa malori mawili, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 8,060,000.

Aidha, taarifa za ndani zinadai kuwa mazingira ya wizi huo yalibainika baada ya mhandisi kutoka katika kampuni ya Nippo -Dai Nippon aliyejulikana kwa jina la Gonai, kuona reki inayotumika kusambaza lami ni moja.

Hatua hiyo, ilimfanya awasiliane na viongozi wenzake ili kubaini tatizo ni nini kutokana na kazi kusuasua na hatimaye kuchukua hatua zilizobainisha kuibwa kwa vifaa hivyo.

Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Ramadhan Kingai, alithibitisha kwa njia ya simu jana juu ya tukio hilo na kusema Athumani amekamatwa na anashikiliwa na polisi Kituo cha Kijitonyama.

Kingai alisema uchunguzi juu ya suala hilo unaendelea na kwamba wakati wowoye mtuhumiwa atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mradi wa upanuzi wa Morocco - Mwenge awamu ya pili, ulitiwa saini na Wakala wa Barabara (TANROADS) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) Macho Mosi, 2019 ukiwa na lengo la kupunguza msongamano wa magari ambao ulikuwapo kwa muda mrefu.



Diwani wa Kata ya Mabwepande, Mhajilina Kassim 'Obama' (kulia), akiongoza wananchi kufanya msako wa nyoka aina ya chatu wanaodaiwa kutishia usalama wa wananchi wa eneo la Kitunda, Mtaa wa Bunju B jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mganga matatani kifo cha mwanawe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamsaka mganga wa kienyeji, Dela Megejua (44), mkazi wa Kijiji cha Mwaningi, Kata ya Bulige Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, kwa madai ya kusababisha kifo cha mtoto wake, Juma Megejua (12).

Mtuhumiwa kumpatia dawa ya kusafisha nyota ambayo inadhaniwa kuwa na sumu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, alisema tukio hilo limetokea Januari 16, mwaka huu majira alasiri nyumbani kwa mtuhumiwa.

Katika tukio hilo, mganga huyo anadaiwa alimpatia mtoto wake dawa akiwa na wenzake wawili walikunywa dawa hiyo ya kienyeji na kuanza kuugua.

Alisema baada ya kuzidiwa watu hao wawili ambao ni Loya Ngusa na Bahati Ngusa wao walizirai papo hapo, kisha kukimbizwa kwenye Kituo cha Afya cha Chela kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Hata hivyo, mtoto wa mtuhumiwa huyo alifariki dunia akiwa nyumbani, na mwili wake umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

"Baada ya kutokea tukio hilo mtuhumiwa alikimbia kusikojulikana, na polisi wanamsaka ili afikishwe katika vyombo vya sheria," alisema Magiligimba.

Aidha, kamanda alitoa wito kwa waganga wa jadi mkoani Shinyanga kuwa na uhakika na matumizi ya dawa zao pamoja na matumizi mazuri ya vibali au leseni.

# ATCL, India zapanua wigo usafiri wa ndege

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limeingia makubaliano ya kimkakati na kibiashara na Shirika la Ndege India, kwa lengo la kupanua mtandao wake kimataifa.

Baada ya kuingia kwa makubaliano hayo, abiria wa ATCL ataweza kukata tiketi moja ya kwenda mji wa Mumbai, India pamoja na miji mingine nchini humo, tofauti na awali abiria walilazimika kukata tiketi mara mbili.

Hatua hiyo italisaidia ATCL kujitangaza kimataifa, itaongeza idadi ya abiria, kuongeza watalii pamoja na kumpunguzia gharama ya mizigo abiria.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu ushirikiano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema: "Baada ya kukamilisha ndani ya nchi sasa tumeanza kuangalia nje. Kwa sasa ATCL inakwenda Mumbai, kupitia ATCL abiria ataweza kukata tiketi moja kuanzia Dar es Salaam hadi mji anakokwenda kama ni Mumbai au New Delh."

Alisema hatua hiyo itampa unafuu wa mizigo abiria, itatusaidia ATCL kupanuka zaidi duniani, pia itatusaidia kujitangaza katika miji ambayo hatufiki. Alisema ATCL inaendelea kujipanua.

"Tunatarajia kuanza safari za kwenda China muda wowote kuanzia sasa, kuna taratibu zinakamilika. Tumeanza na Air India ni matumaini yetu mashirika mengine yatafuata." Alisema Mhandisi Matindi.

Mhandisi Matandi alisema ATCL inakwenda mara nne India ikiwa na abiria wapatao 1,200, hivyo kwa ushirikiano huo idadi itaongezeka.

Naibu Balozi wa India, nchini, R. Chandramouli, alisema wananchi wa India wamekuwa wakitaabika kwa miaka mingi kuja Tanzania moja kwa moja na ndege kwa kukata tiketi mara mbili.

Alisema awali raia wa India waliokuwa wakiishi Tanzania walilazimika kukata tiketi mara mbili wakati wakisafiriki kurudi kwao.

"Ushirikiano huu utakuwa ni wa mafanikio makubwa, ni ushirikiano utakaokuwa na faida kwa nchi zote mbili, hatua hii itakuza undugu uliokuwapo tangu zamani, pia utaongeza idadi ya watalii," alisema Chandramouli.

Aliongeza kuwa kiasi cha biashara kinachofanywa kati ya Tanzania na India ni Dola za Marekani bilioni 1.4, kwa takwimu zilizotolewa hadi Novemba, mwaka jana.

**HABARI KITAIFA**

## Mbunge: Wazazi wanaowaficha ndani wenye ulemavu wasakwe

**Na Dinna Stephano,** MUSOMA

MBUNGE wa Viti Maalum mkoni Mara, Agness Marwa, ameviomba vyombo vya dola kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wazazi na walezi wote wanaowaficha ndani na kushindwa kuwasomesha watoto wenye ulemavu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mjini Musoma alipotembelea na kutoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo chakula na vifaa vya shule katika Shule ya Msingi ya Nyarigamba 'A' katika Manispaa ya Musoma, mkoani Mara.

Alisema kumfungia ndani mtoto mwenye uhitaji siyo tu ni kinyume cha sheria bali pia ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mbunge huyo ambaye yupo katika ziara ya kibunge mkoani Mara, anakutana na makundi mbalimbali ya kijamii ili kuhamasisha shughuli za maendeleo ya kisekta.

"Wazazi wasiwafiche watoto wenye ulemavu wa aina yoyote, serikali inataka kila mtoto asome na wanasome bure," alisema.

"Lakini, mmeniambia hii shule ina changamoto ya choo, mmewashirikisha wazazi kuhusu hili? Kama bado nashauri washirikisheni," alishauri.

Agness alitoa msaada wa kilo 50 za mchele pamoja na vifaa vya shule.

Msaada mwingine alioutoa ni fimbo za kutembelea kwa watu mwenye ulemavu shuleni hapo.

Awali uongozi wa shule hiyo yenye watoto walio na ulemavu na wasio na ulemavu, ulisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto kadhaa.

"Vifaa vya kufundishia baadhi ya wanafunzi hawana sare za shule, uhaba wa madawati pamoja na vyoo," alisema Sista Grace Damas, mwalimu wa kitengo cha elimu maalum.

**Lakini, mmeniambia hii shule ina changamoto ya choo, mmewashirikisha wazazi kuhusu hili? Kama bado nashauri washirikisheni.**

# Watumishi Tume ya Kurekebisha Sheria wapewa ushauri kustaafu

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MWENYEKITI wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Jaji mstaafu January Msofe, amewataka watumishi wa tume kujipanga na kuanza maandalizi ya kustaafu wakati wakiwa kazini.

Jaji mstaafu Msofe alisema hayo wakati akifunga mkutano wa 15 wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Kurekebisha Sheria lililofanyika mwishoni mwa wiki katika ukumbi wa Chuo cha Benki Kuu (BoT) jijini Mwanza.

Aliwataka watumishi wa tume kuacha kubweteka wakati wakiwa kazini na kuanza kujipanga kwa kujiandaa kwa maisha ya kustaafu na kusisitiza kuwa kuna baadhi ya watumishi waliadhirika mara tu baada ya kustaafu kutokana na kutojiandaa mapema.

"Wapo walioadhirika na kustaafu bila ya kuwa na hata kibanda, hivyo haya maisha tusipoangalia yanatudanganya na unabweteka," alisema Jaji mstaafu Msofe.

Aidha, aliwataka watumishi wa tume hiyo kuzingatia mafunzo waliyoyapata kupitia mada za Mfuko wa Uwekezaji wa UTT pamoja na Mfuko wa Pembejeo aliyoyaeleza kuwa yalilenga kuwandaa watumishi hao kustaafu.

Mkutano wa 15 wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ulifanyika kwa siku mbili na kufunguliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Profesa Sifuni Mchome, aliyetaka tume mbali na mambo mengine, kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria kwa lengo la kuivusha nchi katika uchumi wa kati wa juu kutoka uchumi wa kipato cha kati iliyopo sasa.



Mhasibu kitengo cha Pensheni kutoka Makao Makuu Charles Kuisale, akiendesha zoezi la uhakiki wazee wastaafu katika manispaa ya Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ruksa wakulima kuuza mazao nje

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

SERIKALI imeruhusu mazao ya chakula kuuzwa nje ya nchi ili kutoa fursa kwa wakulima kunufaika na mazao mbalimbali wanayoyazalisha.

Imesema kuwa itakuwa ikitoa vibali kwa wafanyabiashara wa mazao.

Hayo alisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, walipokuwa kwenye ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya kilimo iliopo mkoani Morogoro, ambapo aliwataka wakulima kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi.

"Serikali kupitia wizara yangu imeamua kufungua fursa kwa wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi kulingana na mahitaji ya soko la nchi husika ili kuwapa faida wakulima hao na kuwaimarisha kiuchumi zaidi," alisema Kusaya.

Kusaya alisema Wizara ya Kilimo inawataka wafanyabiashara wa mazao hasa ya chakula kujitokeza kufanya biashara nje ya nchi kwani serikali itakuwa bega kwa bega kutoa vibali kwa wafanyabiashara wanaotaka kuuza mazao yao nje.

Katibu Mkuu huyu alisema serikali imeruhusu mazao kuuzwa nje nchi ili kutoa fursa ya kuongeza soko kwa wakulima kupata faida zaidi kutokana na kutumia nguvu nyingi katika uzalishaji wa mazao mbalimbali hasa ya chakula.

Aidha, katibu huyo amewataka wakulima wa mazao ya chakula kuongeza bidii ya uzalishaji wa mazao hayo ili kupata faida kubwa inakayowafanya wanufaike na kilimo chao kutokana na mauzo ya mazao yao kwenye soko la dunia.

Kutokana na tamko hilo wakulima wa mazao hayo mkoani hapa wameipongeza serikali kwa kuruhusu mazao yao kuuzwa nje ya nchi ambapo walisema kutasaidia sana kuondokana na changamoto ya kukosekana kukosa masoko ya uhakika.

Awali wakulima wao walimweleza Katibu Mkuu huo wa Wizara hiyo juu ya changamoto mbalimbali zilizokuwa zinawakabili ikiwamo ya soko na upatikanaji wa pembejeo hali iliyomlazimu Kusaya kuruhusu mazao kuuzwa nje ya nchi.

Shelua Ramadhani, aliishukuru serikali kwa kuliangalia suala hilo kwa jicho la tatu na kwamba kupitia tamko hilo wakulima wengi watanufaika na uzalishaji wa mazao yao kila mwaka.

Kwa upande wake Agnes James alisema kutokana na serikali kuruhusu mazao kuuzwa nje ya nchi kutafungua fursa kwa wakulima wengi kulima kwa wingi kwani watakuwa na soko la uhakika zaidi na kunawafanya wapate faida.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuanze mikakati kufikia soko la wenye COVID-19

**RAIS** John Magufuli, ametoa wito kwa Watanzania kuzalisha kwa wingi hasa mazao ya chakula ili kuyauzia mataifa ambayo yameathirika na COVID-19 ambayo bila shaka ni nchi za Afrika.

Alilozungumza Rais ni jambo linaloonyesha wazi kuwa serikali imeazimia kuwaunga mkono wakulima na wazalishaji wakiwamo wasindikaji na viwanda ambavyo vina fursa ya kuuza kwa tija kupitia angalizo hilo.

Ni wazi kuwa ni fursa ambayo inahitaji uwekezaji kuanzia sasa ambao utafanikisha kulima na usindikaji wa nafaka kama mahindi kupata unga wa madaraja mbalimbali, mchele wa viwango na madaraja tofauti, kadhalika matunda na mboga.

Tunatamani kuona maelekezo ya Rais yakianza kufanyiwa kazi sasa kwa vile kuna mazao ya kutosha yanayoweza kuuzwa kwa tija kwa mataifa kama Malawi, Rwanda, Burundi, Zambia, Congo DRC na Sudan Kusini.

Mauzo yanaweza kufanyika sasa iwapo kuna wakulima wenye akiba ya nafaka kama mchele, ngano, mtama na mahindi. Aidha, kama kuna mbegu za mafuta kama korosho na karanga. Kuna jamii ya kunde hasa choroko, kunde, dengu, mbaazi na maharage.

Lakini, vipo viungo kama vitunguu vya aina mbalimbali, yapo matunda kuanzia matikiti maji, nyanya, mafenesi, maparachichi na ndizi. Si hivyo pekee kuna mifugo kama nyama na hata maziwa ambavyo vyote vinaweza kuuzwa kwa tija na wakulima wakanufaika na fursa hiyo ya kuwapo kwa soko la chakula kwa mataifa yaliyoathirika na COVID -19.

Kama Rais alivyosema ni muhimu Watanzania wakazalisha kwa wingi mazao ya chakula, ili kunufaika na soko lililoko kwenye mataifa ambayo hakuna chakula kutokana na wananchi kufungiwa ndani kuepuka kusambaa kwa maradhi ya corona.

Rais anasisitiza umuhimu wa kutumia mvua zinazoendelea kunyesha na kukumbusha kuwa hivi sasa maeneo mbalimbali ya nchi hii yana mvua hivyo watu waanze kulima mazao hasa ya chakula tena kwa wingi ili baadaye yauzwe kuwasaidia wenzetu ambao wanashindwa kulima kutokana na corona.

Wakuu wa Wilaya na Mikoa waisikie kauli ya Rais kuhamasisha kilimo, kwa mfano mijini kuna mapori mengi na watu hawayatumii kwa kilimo, kwa mfano Dar es Salaam, kuna mashamba makubwa ambayo hayajaendelezwa, mathalani kuweka nyumba za makazi, ni vyema viongozi wa serikali za mitaa wakahimiza watu kuruhusiwa kuyalima kupanda mazao ya muda mfupi kama mihogo, ndizi, viazi, kunde, mbaazi na choroko ambayo wanaweza kuuza na kunufaika na fursa hiyo ya 'soko la corona.'


Ni wakati pia wa kuangalia jinsi bora ya kusindika bidhaa hizo ili kunufaika na soko hilo. Ndiyo maana tunawashauri wadau wa uwekezaji kwenye viwanda likiwamo Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TRIDO), Viwango la Taifa (TBS) na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuweka mikakati ya namna bora ya kuwawezesha wananchi kunufaika na soko la corona lililoko nje ya nchi.

Pamoja na jitihada hizo Mamlaka ya Uuzaji Nje ya Nchi (EPZA) ina nafsi ya kusaidia kufanikisha juhudi hizo kwa kuwezesha uwekezaji na hata kutoa nafasi zinazoweza kutumiwa kama viwanda ili kuzalishaji bidhaa zinazotokana na kilimo, ufugaji na uvuvi na kusindika mathalani, pamba ili kuzalisha nguo zinazoweza kupelekwa kwa nchi zenye corona.

Tunaona kuwa ni sasa tuwe na mikakati ya kitaifa ya kuandaa mipango, kuisimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo ya kuuza nje kwa kuwa ni soko lisilo na upinzani linaloweza kuwaondolea Watanzania wengi umaskini wa kipato.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# 'Kula urefu wa akili yako, usiibe mitihani'

**BARAZA** la Mitihani Taifa (NECTA), limefuta matokeo ya watahiniwa 215 waliobainika kufanya udanganyifu katika mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana.

Katibu Mtendaji wa Baraza, Dk. Charles Msonde, aliyesema hayo wakati akitangaza matokeo ya kitaifa ya upimaji wa maarifa kwa darasa la nne, kidato cha pili na cha nne kwa mitihani huo wa mwaka jana.

Udanganyifu wa mtihani umekuwa jambo la kawaida katika shule mbalimbali nchini, ingawa baadhi ya watuhumiwa wamewahi kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Hatua nyingine ambazo zinachukuliwa, ni pamoja na kutoa onyo kabla ya kufanyika kwa mitihani, lakini bado udanganyifu umeendelea kujirudia.

Kwa mfano, mwaka jana, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Kagera, ilikaririwa na vyombo vya habari ikitangaza kuwashikilia watu 67 wakiwamo wanafunzi 59.

Wanafunzi hao walikuwa ni wa vyuo viwili vya ufundi stadi (VETA), wakuu wa vyuo hivyo na wakufunzi sita, kwa tuhuma za kufanya udanganyifu katika mitihani na matumizi mabaya ya ofisi.

Kwa mujibu wa TAKUKURU mkoani humo, walimu walishirikiana na wanafunzi na kutengeneza makundi mawili ya mtandao wa 'whatsapp' ambayo yalitumika kutuma majibu.

Si hapo tu, mwishoni mwa mwaka jana, NECTA ilitangaza kuwafutia matokeo watahiniwa 1,059 kutoka shule 38 zilizofanya udanganyifu katika mitihani ya kuhitimu darasa la saba mwaka huo.

Nani yuko nyuma ya udanganyifu huo? Kwanini sasa limekuwa kama jambo la kawaida, kila unapofanyika mtihani, wajanja wachache wanapenyeza na kufanya udanganyifu na kuvuruga lengo la kutaka kila mwanafunzi afaulu kulingana na uwezo wake darasani?

Udanganyifu kwenye mitihani nchini umekuwapo na jitihada za kuukomesha zinaendelea, hivyo kuna haja ya kutafuta mbinu nyingine zaidi za kukabiliana nao.

Bila kuwa na ubunifu zaidi kukabiliana na udanganyifu huo, kuna hatari ya kuzalisha wasomi mbumbumbu ambao hawatakuwa na faida kwa taifa lao, kwa kuwa watakuwa na sifa ambazo haziendani na uwezo wa kielimu.

Umefika wakati wadau wa elimu kuanzia wazazi na walezi kuachana na kujiingiza kwenye udanganyifu wa mitihani unaosababisha watoto wao wafaulu japo hawakustahili.

Kila mmoja akitimiza wajibu wake inavyotakiwa, hakutakuwa na udanganyifu unaojirudia kwenye mitihani na kusababisha kiwango cha elimu kushuka kwa kupata wasomi wasio na sifa.

Wadau wa elimu wasiweke pamba masikioni, bali wasikilize kile ambacho kimekuwa kikielezwa na NECTA ili watoe mchango katika kukomesha vitendo hivyo, ambavyo vinadhalilisha elimu.

Haipendezi kuona watu wachache wakiendelea kuwaharibia watoto maisha yao ya baadaye kwa kushirikisha katika udanganyifu wa mitihani, ambao mwisho wake kufutiwa matokeo ya mtihani.

Suala la kuimarisha usimamizi wa mitihani ni la muhimu ili usiwepo mwanya wa kuwafanya wadanganyifu kuendelea kuutumia kwa manufaa yao na kusababisha wanafunzi kufutiwa matokeo.

Kasi ya TAKUKURU kunasa watuhumiwa iendelee kuongezeka, ili kuziba mianya ya wahusika na kuacha kila mwanafunzi afaulu mitihani kulingana na uwezo wake wa darasani alionao.

Watoto ndiyo raia na taifa la kesho, hivyo kuwapa wote elimu ni jambo muhimu lisilo na mbadala, lakini unapoingizwa udanganyifu katika mitihani, hiyo ni sawa na kuwaharibia ndoto zao za baadaye.

Inaumiza kuona mwanafunzi amesotwa kwa miaka yote minne akiwa sekondari, halafu badala ya kufanya mtihani inavyotakiwa, anajiingiza kwenye udanganyifu ili apate ufaulu usiolingana na uwezo wake.

Waswahili wana msemo kwamba; 'mbuzi hula kulingana na urefu wa kamba yake', hivyo hata wanafunzi nao hawana budi kushinda au kufaulu mitihani kulingana na uwezo wa akili zao.

Hivyo wale ambao watafanya mitihani yao kuanzia sasa wajifunze kwa wale ambao wamefutiwa matokeo ili nao yasije kuwakuta kwa kukubali kuingia kwenye mtego huo wa udanganyifu.

HABARI KITAIFA

# Mvuvi afariki akivua samaki

**Na Said Hamdani,** LINDI

MVUVI mkazi wa Kijiji na Kata ya Nachunyu, Halmashauri ya Mtama, Wilaya na Mkoa wa Lindi, Hafidhi Ally (20) amefariki dunia alipokuwa akivua kwenye Bahari ya Hindi.

Taarifa kutoka katani humo na kuthibitishwa na Jeshi la Polisi mkoani humo, zinaeleza kwamba Hafidhi Ally alipatwa na mauti Januari 14, mwaka huu.

Baadhi ya mashuhuda, wakiwamo jamaa na ndugu wa Yusufu Ally, Maulid Daudi na Mwanabibi Hemedi, walisema siku hiyo asubuhi, Ally aliondoka nyumbani kwake kwenda Baharini kuvua, lakini hakurejea nyumbani.

Pia walieleza kwamba kitendo cha kutorejea kuliwapa hofu ndipo zoezi la kumsaka lilipoanza na kufanikiwa kuupata mwili wake Januari 17, mwaka huu, ukiwa ndani ya mtumbwi aliokuwa akitumia kuvulia samaki.

Walisema mwili wa Ally walifanikiwa kuupata juzi (Januari 17) ukiwa ndani ya mtumbwi ukielea baharini.

Aidha, walieleza kwamba licha ya kuukuta mwili huo ukiwa ndani ya mtumbwi huo pia walikuta samaki aina ya changu na chewa wasiopungua kumi aliokuwa amewavua siku hiyo.

"Tunaweza kusema ni bahati tu kwani tungekuta mwili unaelekea majini na mtumbwi upo peke yake, tungesema labda dhoruba ya upepo, lakini tumemkuta ndani ya chombo alichokuwa anakitumia," alisema Yusufu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya, alithibitisha kutokea kwa kifo cha mvuvi huyo, huku akitoa tahadhali kwa wavuvi kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Hali Hewa (TMA) kutokana na upepo mkali unaoendelea kuvuma kwenye Bahari ya Hindi.

**Tunaweza kusema ni bahati tu kwani tungekuta mwili unaelekea majini na mtumbwi upo peke yake, tungesema labda dhoruba ya upepo, lakini tumemkuta ndani ya chombo alichokuwa anakitumia.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## MWITO WA KUTOA MAONI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Saint Parts Co. Ltd<br>S.L.P. 77903<br>Dar es Salaam | Eneo la Shaurimoyo, Manispaa ya Iala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Kenichi Tenaya<br>(Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 2. | Furahisha Franci Msigwa – FM Filling Station<br>S. L. P 497<br>Makambako | Kiwanja Na. 84, Kitalu 'G', Eneo la Uyole, Jiji la Mbeya | Furahisha Franci Msigwa<br>(Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | ATN Petroleum Kigamboni Tuamoyo<br>S.L.P. 863<br>Morogoro | Kiwanja Na. 1083, Kitalu 'D', Eneo la Tuamoyo, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Abdulatif Taalib Mohamed<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | ATN Petroleum Kigamboni Tuamoyo<br>S.L.P. 863<br>Morogoro | Kiwanja Na. 81 & 82, Eneo la Wazo, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Abdulatif Taalib Mohamed<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Engen Masaki Service Station<br>S.L.P. 78470<br>Dar es Salaam | Kiwanja Na. 2056, Kitalu 'AT', Eneo la Masakai, Barabara ya Chole,Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Abdallah Kijangwa<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Malimaua Filling Station<br>S. L. P. 81<br>Chemba, Dodoma | Kijiji cha Itiso, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma | Juma Yusufu Kishari<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Nuroil Petrol Station<br>S. L. P. 22<br>Nguruka, Kigoma | Kiwanja Na. 125, Kitalu "G", Wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora | Issa Mohamedi Ally<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 8. | Marwa Munanka Chacha<br>S. L. P. 121<br>Igunga, Tabora | Kijiji cha Konkilangi, Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida | Marwa Munanka Chacha<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | AMI Tanzania Limited<br>S.L.P. 9041<br>Dar es Salaam | Kiwanja na. 27/2/3, Kitalu '234', eneo la Mabibo, Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam. | Augustine Gasaza Ayishashe<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 10. | Wakulima Tea Company<br>S. L. P 700<br>Tukuyu | Eneo la Katumba Kiwandani - Tukuyu, Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya | Benjamin Aloyce<br>(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 11. | Edith Kibali Miaka Elfu Moja<br>S.L.P 92<br>Mtwara | Kiwanja Namba 23, Eneo la Sokoni, Mtwara Mjini | Amon Sengati<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 12. | Tully Hallan Musyani<br>S. L. P 2099<br>Mbeya | Eneo la Ilomba, Mbeya Mjini, Wilaya ya Mbeya, Mkoa wa Mbeya | Tully Hallan Musyani<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 13. | Tema General Traders<br>S. L. P 2947<br>Mbeya | Eneo la Uyole, Mbeya Mjini, Wilaya ya Mbeya, Mkoa wa Mbeya | Diana Tesha<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 14. | Mohamed Sudy Ally<br>S. L. P 45<br>Sumbawanga | Eneo la Mashine – Mazwi, Manispaa ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa | Mohamed Sudy Ally<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 15. | Hamad Faki Hamad<br>S. L. P 149<br>Mbeya | Eneo la Soweto, Kata ya Ruanda, Jiji la Mbeya | Hamad Faki Hamad<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 16. | Salum Hemed Saud<br>S. L. P 32<br>Sumbawanga | Eneo la Katandala, Manispaa ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa | Salum Hemed Saud<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 17. | JJM GES<br>S. L. P 1352<br>Moshi | Kiwanja Namba 111, Kitalu "AAA", Eneo la Bondeni, Kata ya Korongoni, Halmashauri ya Manispaa Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro | Mariam Anselimu Olomi<br>(Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |

**Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-4, Nukushi: +255 26 2329005

Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz

# Kiswahili chatumika asilimia 70 kesi mahakama za mwanzo

**Na Elizabeth Zaya**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, amesema matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mahakama zamwanzo nchini yamefikia asilimia 70 katika uendeshaji wa shughuli zake.

Aidha, amesema katika Mahakama nyingine ikiwamo za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Rufani bado wanaendelea kukamilisha utaratibu wa kuhakikisha nazo zinatumia lugha hiyo katika uendeshaji wa shughuli zake zote.

Jaji Mkuu alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanayotarajia kuanza Januari 23 hadi Februari Mosi mwaka huu.

"Kubadili matumizi ya lugha ya kutumia mahakamani kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili bado kunahitaji umakini mkubwa kufikia katika hatua hiyo, lakini hili la kuitumia ni muhimu, tumefanikiwa katika Mahakama za Mwanzo," alisema Prof. Juma.

"Katika mahakama hizi nyingine zilizobaki pamoja na kwamba bado zinatumia lugha ya Kiingereza, lakini kunapokuwa hakuna mawakili mara nyingi mazungumzo yanakuwa ni Kiswahili, isipokuwa rekodi zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza."

"Na tuliongea na Waziri kwamba suala la kubadili lugha ya kutumia mahakamani kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kunahitaji umakini mkubwa kwa sababu wanasheria wamesoma kwa lugha hiyo na lugha ya sheria ni Kiingereza ambacho kina maneno mengi sana, lakini tunatakiwa tutoke huko kwenye karne ya 20."

Mwaka jana, Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, alizitaka Mahakama kuangalia uwezekano wa kutumia lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa shughuli hizo za Mahakama.

Aidha, Prof. Juma alisema maadhimisho hayo ya Wiki ya Sheria yanatarajiwa kufunguliwa kwa matembezi yatakayoongozwa na Makamu ya Rais, Samia Suluh Hassan na kufungwa na Rais John Magufuli Februari Mosi, mwaka huu, jijini Dodoma.

Mbali na Dodoma, pia alisema katika wiki hiyo yote, yatakuwa yanaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Prof. Juma alisema maadhimisho hayo yataambatana na miaka 100 ya Mahakama Kuu, na kwamba kaulimbiu yake inasema "miaka 100, Mahakama Kuu, mchango wa Mahakama katika kujenga nchi inayozingatia uhuru, haki, udugu amani, ustawi wa wananchi kati ya mwaka 1920 na mwaka 2020."

Alisema kaulimbiu hiyo inalenga kuonyesha maudhui ya ufanisi wa utoaji haki katika kipindi hicho cha miaka 100 ya mahakama.




Naibu Waziri wa Michezo, Abdallah Ulega (wa pili kulia), akimkabidhi Abdul-aziz Abdulla (katikati) cheti cha udhamini wa masomo 'Scholarship' uliotolewa kwa vijana waliofanya vizuri katika mashindano ya ligi ya taifa ya mpira wa kikapu ijulikanao CRDB Bank Taifa Cup, yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka jana. Wengine; kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile, Mjumbe wa Bodi ya Benki ya CRDB, Martin Warioba na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania, Phares Magesa. Benki ya CRDB imetoa udhamini wa masomo kwa vijana 26 wenye jumla ya Sh. milioni 50. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kila siku ajali mbili Z.Victoria

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KUNA wastani wa ajali mbili hadi tatu kila siku kwenye Ziwa Victoria eneo la Tanzania, ambazo wakati mwingine zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

Kutokana na hali hiyo, serikali imejikita katika kutoa elimu ili kuhakikisha ajali za majini katika ziwa hilo zinapungua. Akizungumza wakati wa kutoa elimu kuhusu usalama majini kwa wakazi wa Kisiwa cha Miembeni, Kata ya Sega mkoani Geita jana, Ofisa wa Kitengo cha Uratibu na Uokozi Ziwa Victoria, Joseph Mkumbo, alisema wastani wa ajali mbili hadi tatu hutokea kila siku katika ziwa hilo upande wa Tanzania.

"Kwa sasa, tuna wastani wa ajali mbili hadi tatu ambazo hutokea kwenye Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania na kugharimu maisha ya watu. "Sababu kuu za kutokea kwa ajali hizo ni ubovu wa vyombo vya usafiri pamoja na ubebaji wa abiria na mizigo kupita kiasi.

"Watu wengi ambao wanapoteza maisha kutokana na ajali kwenye ziwa hili, ni wale wasiotumia vifaa vya uokoaji kama maboya," alisema.

Ofisa Mfawidhi wa Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) Mkoa wa Geita, Rashid Katonga, alisema kuna matatizo mengi kwa watumiaji na wamiliki wa vyombo vya majini, akidokeza kuwa wengi wao wamekuwa hawazingatii ubora wa vyombo kutotumia vifaa vya uokoaji bila kujua athari zake.

"Tunatoa elimu kila kona kuhakikisha wananchi wako salama, tunasajili vyombo vya majini ikiwamo mitumbwi ya uvuvi na boti za abiria tukilenga kuhakikisha vyombo husika vina ubora na ni salama kwa watumiaji wake majini.

"Watu wengi hupoteza maisha kwenye ziwa kutokana na kutozingatia taratibu za kiusalama, tunawaelimisha na hii kwa Geita imesaidia kupunguza vifo pale ajali inapotokea," alisema.

Ofisa huyo wa TASAC alibainisha Mkoa wa Geita unakadiriwa kuwa na boti zaidi 1,000 zinazotoa huduma ya usafirishaji katika Ziwa Victoria.

Kati yake, 750 zimesajiliwa, 48 zikitoa huduma za usafirishaji majini wakati nyingine nyingi zikitumika kwenye shughuli za uvuvi.

# Wanyamapori kuhifadhiwa kwenye kisiwa Ziwa Nyasa

**Na Gideon Mwakanosya,** NYASA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kupeleka wanyama kwenye kisiwa cha Lundo Ziwa Nyasa, Wilaya ya Nyasa.

Akizungumza kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Mndeme alisisitiza kuwa kupelekwa kwa wanyama katika kisiwa hicho, kutasaidia kuongeza vivutio kwa watalii kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana Wilaya ya Nyasa ambayo imetangazwa kuwa kitovu cha utalii katika Mkoa wa Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa pia aliwaagiza wadau wa utalii na uhifadhi zikiwamo TAWA na TANAPA kuchukua jukumu la kutoa elimu ya uhifadhi na utalii kwa wananchi hasa wa Mkoa wa Ruvuma kuhusu umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchochea uchumi. Mndeme pia aliagiza ushoroba na mapito ya wanyama katika Mkoa wa Ruvuma yaheshimiwe na kulindwa kwa sababu ni moja ya rasilimali za nchi na ameagiza wananchi wote waliovamia maeneo hayo waondolewe haraka.

Kufuatia maagizo hayo, wadau wa utalii mkoani Ruvuma wakiwamo TAWA, TANAPA na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wameanza kuchukua hatua ikiwamo azma ya kuanzisha hifadhi ya kufuga wanyamapori katika kisiwa cha Lundo, kifuga ndege katika kisiwa cha Mbambabay (Zambia).

Mshauri wa Maliasili na Utalii Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe, alisema wanatarajia kuanzisha Hifadhi ya Mbambabay ambayo inajumuisha visiwa vya Lundo, Mbambabay na milima ya Mbamba, Tumbi na Ndengere wilayani Nyasa.

Challe aliitaja Hifadhi ya Mbambabay itakuwa na ukubwa wa eneo la hekta 597, na kwamba maeneo hayo yanafaa kwa kufuga wanyamapori na ndege.

Hata hivyo, alisema kati ya hekta hizo, mlima Mbamba una eneo lenye ukubwa wa hekta40, mlima Tumbi hekta 110, kisiwa Mbambabay chenye hekta 27, kitakuwa maalum kwa ufugaji wa ndege na kisiwa cha Lundo chenye ukubwa wa hekta 20, TAWA inatarajia kupeleka wanyamapori jamii ya swala.

"Milima na visiwa hivi vimejaaliwa kuwa na uoto mzuri wa miombo, mawe yanayozunguka visiwa hivi na milima kando kando ya ziwa yana hifadhi samaki adimu wa mapambo zaidi ya aina 400," alibainisha Challe.

Kwa mujibu wa Challe, eneo la Hifadhi ya Mbambabay ni muhimu sana kwa upande wa Tanzania husasan katika matumizi ya shughuli za utalii kama vile utalii wa kuvua samaki, kupiga mbizi, yatching, utalii wa kuendesha mitumbwi na kuweka kambi kwenye fukwe.

Mtalaam huyo wa uhifadhi alisema eneo hilo likihifadhiwa litatumika kwa ajili ya mazalia ya samaki, hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi.

"Mbambabay ikihifadhiwa inaweza kuleta ushindani kibiashara nchini kwa sababu katika nchi yetu hakuna eneo linaloweza kutoa mchanganyiko mzuri wa huduma za kitalii kama zitakazotolewa katika eneo hili," alieleza.

HABARI KITAIFA

# Manispaa Morogoro yaagizwa usafi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mwita Waitara, ameiagiza Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kusimamia usafi na kuweka mikakati itakayosaidia wananchi kuona jukumu la usafi ni la wote.

Waitara alitoa agizo hilo mjini hapa wakati wa ziara ya ukaguzi wa dampo la taka la Manispaa hiyo lililopo eneo la Kata ya Mafisa.

Alisema suala la usafi wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi, lakini tatizo kubwa linalojionyesha ni baadhi ya halmashauri haziwashirikishi wananchi moja kwa moja, na wakati mwingine kupanga mipango ambayo imekuwa ikiwakandamiza wananchi, hivyo kugomea suala la usafi.

Hata hivyo, alipongeza manispaa hiyo kwa mipango mizuri na kuitaka iongeze nguvu katika ufuatiliaji wa mradi mpya wa ujenzi wa dampo la kisasa.

Waitara alisema hatua za kuanza kutekeleza ujenzi wa dampo jipya la kisasa, ni la kupongezwa kwa vile andiko lake limeshawasilishwa kwake na moja kazi yake ni kusukuma ili fedha ziweze kutolewa kwa kuwezesha kuanza kwa ujenzi.

"Mtakapoletewa fedha za ujenzi wa dampo hilo la kisasa, niwatake tu lizingatie miundombinu yote, lisiwe kama hili la kienyeji kwani hapa tushakosea," alisema alipotembelea dampo la taka la sasa.

Naibu Waziri aliitaka Manispaa hiyo kuhakikihsa wakati wanajiandaa na ujenzi wa dampo jipya, lililopo kwa sasa lifanyiwa maboresho ili mazingira rafiki taka zisibaki nje ya dampo.

"Hakikisheni mnatengeneza mifereji ya maji ya mvua, na maji ya sumu yaende katika mkondo sahihi wa maji hatarishi na bila kusahau kuruhsu maji hayo baada ya kujiridhisha na vipimo vinavyotakiwa," alisema Waitara.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheilla Lukuba, alisema Manispaa imetenga bajeti ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya ununuzi wa gari la taka ili kuongeza nguvu katika suala la usombaji wa taka ngumu kutoka kwenye vituo mbalimbali wa uhifadhi wa muda wa taka.

Ofisa wa dampo, Alex Roman, alisema hali ya mazingira na usimamizi wa taka katika dampo la sasa bado kuna changamoto kutokana na kuongezeka kwa wingi wa taka kutokana na ongezeko la idadi ya watu pamoja na shughuli za uzalishaji wa taka viwandani.

# Wafanyabiashara Zanzibar watakiwa kusajili biashara

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAIMU Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Mudrik Soraga, amewataka wafanyabiashara kusajili biashara zao hatua itakayowawezesha kutambuliwa rasmi na kuwa walipa kodi ili kuchangia maendeleo ya taifa.

Alisema hayo alipokuwa akilifungua Tamasha la Saba la Biashara la Zanzibar kwenye viwanja vya Maisara Manispaa ya Zanzibar, ambalo hufanyika kila mwaka kwa ajili ya kusherehekea Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo kwa mwaka huu yametimiza miaka 57.

Soraga ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, aliwasihi wafanyabiashara kuwa na utamaduni wa kushiriki matamasha mbalimbali ya biashara ya ndani na nje ili kuwaongezea uzoefu hatua itakayowawezesha kupanua wigo wa soko la bidhaa zao na kujiongezea kipato wao binafsi na taifa kwa ujumla.

**Benki yetu ni wadau wakuu wa viwanda na wafanyabiashara wadogo wadogo hivyo ili kuboresha mustakabali wao tunalazimika kuwa na huduma bora zaidi kwa wateja na hata taasisi hususani za Kijamii.**

"Tuna azma ya kuwaalika wafanyabiashara wa mataifa mengine kushiriki tamasha hili katika miaka ijayo hatua itakayolifanya kuwa la Kimataifa na kuongeza wigo kwa wafanyabiashara wa ndani kujifunza zaidi," alisema Soraga.

Aidha, katika hafla hiyo, Soraga alikabidhi tuzo kwa Benki ya NMB na taasisi kadhaa ambazo zilidhamini tamasha hilo la Saba la Biashara la Zanzibar.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Zanzibar, Abdalla Duchi, alisema benki hiyo itaendelea kutoa huduma bora zaidi kwa lengo kukidhi mahitaji ya wateja wake ili kwenda sanjari na sera ya Zanzibar ya uchumi wa buluu.

"Benki yetu ni wadau wakuu wa viwanda na wafanyabiashara wadogo wadogo hivyo ili kuboresha mustakabali wao tunalazimika kuwa na huduma bora zaidi kwa wateja na hata taasisi hususani za Kijamii," alisema Duchi.

Pamoja na hayo, aliishukuru Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kwa kuandaa tamasha hilo kwa kuwa limetoa fursa kwao (NMB) kujifunza zaidi pamoja na kupata wigo mzuri wa kuonesha huduma zao.

Tamasha la Biashara la Saba la Zanzibar lilikuwa na washiriki 360 lililofungwa Jumapili Januari 17, mwaka 2021 lilifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Januari 6 mwaka 2021.



Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Zanzibar, Abdalla Duchi (kushoto), akipokea cheti kutokana na benki hiyo kudhamini maonyesho hayo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrik Soraga ambaye ni Kaimu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhakiki malipo pensheni wawagusa wazee

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZEE wastaafu mkoani Shinyanga, wameanza kuhakikiwa ili kupata taarifa zao sahihi, na kuendelea na zoezi la ulipwaji wa pensheni zao kila mwezi.

Unahusisha kuwaondoa ambao wameshafariki, ili kutoendelea kulipa malipo hewa.

Mhasibu kutoka Hazina ndogo mkoani Shinyanga, Richard Peter, alisema jana kuwa zoezi hilo la kuhakiki wazee wastaafu litadumu kwa wiki nzima.

Alisema wanaendesha zoezi hilo, ili kupata taarifa sahihi za wazee ambao ni wastaafu, na kuwaingiza kwenye mfumo wa mtandao, na kuwaondoa wale ambao wameshafariki dunia, na kusitisha malipo hewa.

"Zoezi hili la kuhakiki wazee wastaafu mkoani Shinyanga limeanza na litaendeshwa hadi Ijumaa, lengo ni kupata taarifa sahihi za wazee ambao wanastahili kulipwa pensheni, na kuondoa malipo hewa ya wazee ambao wameshatangulia mbele za haki," alisema Peter.

Baadhi ya wazee wastaafu ambao wamefika kuhakikiwa taarifa zao, wakiwamo Gideoni Ruhori na Ruth Jonasani, kwa nyakati tofauti walipongeza zoezi hilo namna linavyoendeshwa hasa kwa mfumo wa mtandao, na kwamba litawasaidia kuendelea kulipwa mafao yao bila vikwazo.

# Waziri Ummy awaahidi neema w'biashara vyuma chakavu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, ametangaza neema kwa wajasiriamali wanaokusanya, kuhifadhi na kusafirisha vyuma chakavu kwa kuahidi kwamba muda wa upatikanaji kibali utapunguzwa.

Pia amesema muda wa kibali kuwa halali utarefushwa na kuwa miaka mitatu. Hata hivyo, hakusema muda utapunguzwa kwa kiasi gani. Kwa sasa kibali kinapatikana kati ya miezi mitano na saba na uhai wa kibali ni mwaka mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam baada ya mkutano uliotishwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Joseph Malongo na kuwahusisha wadau wa vyuma chakavu pamoja na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Waziri Mwalimu, alisisitiza kuwa serikali inakusudia kuiboresha biashara hiyo na moja ya hatua itakayochukuliwa ni kupunguza muda wa upatikanaji wa vibali.

Wizara imelenga kuiboresha biashara hii ya vyuma chakavu kwa kuanza na kupunguza muda wa upatikanaji wa vibali uwe muda mfupi ili kuwaondolea usumbufu wafanyabiashara na kurefusha muda wa vibali kutoka mwaka mmoja kwa sasa mpaka miaka mitatu," alisema.

**Viwanda vinahitaji malighafi za kutosha na miongoni mwa mikakati iliyopo ni kuhakikisha malighafi hizo zinapatikana kupitia urejelezaji wa vyuma chakavu; tumejipanga kuja na maboresho ya kanuni ili kuwa na uhakika zaidi wa upatikanaji wa malighafi hizo hususani chuma.**

Waziri aliwataka wafanyabiashara hao kulinda miundombinu hasa reli, majengo, nyaya za simu na umeme pamoja na madaraja.

"Wizara inaitazama biashara hii kuwa miongoni mwa biashara muhimu inayochangia ukuaji wa pato la taifa na pia biashara hii inasaidia kusafisha mazingira yetu."

Lakini ufanyaji wa biashara lazima uende sambamba na utunzaji wa mazingira," alisema Mwalimu.

Alieleza kuwa adhabu watakazopewa wafanyabiashara ambao watakiuka utaratibu uliopo kwa kuharibu miundombinu ni pamoja na kufutiwa kwa vibali vya kufanya biashara hiyo.

"Tunawatazama nyie kama watu muhimu kwa uchumi wa nchi. Lakini hiyo isiwe sababu ya waharibifu wa miundombinu na serikali kushindwa kuchukua hatua," alieleza na kuongeza:

"Tutachukua hatua kali ikiwamo kufutiwa vibali vya ufanyaji wa biashara ya vyuma chakavu pamoja na kupelekwa mahakamani kama wahujumu uchumi."

Katibu Mkuu wa Wizara Malongo alisema serikali imepanga kuboresha biashara hiyo kutoka na umuhimu wake kwa taifa, na kwamba uboreshaji ni sehemu ya utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa viwanda.

"Viwanda vinahitaji malighafi za kutosha na miongoni mwa mikakati iliyopo ni kuhakikisha malighafi hizo zinapatikana kupitia urejelezaji wa vyuma chakavu; tumejipanga kuja na maboresho ya kanuni ili kuwa na uhakika zaidi wa upatikanaji wa malighafi hizo hususani chuma," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema watatumia maoni ya mkutano huo kufanya marekebisho ya kanuni ili kuifanya biashara hiyo kuwa rafiki kwa wadau.

Mkutano uliibua changamoto kadhaa ikiwamo kuchelewa kupatikana kwa vibali pamoja na gharama kubwa za vibali hivyo. Tutaendelea kukutana na wadau ili tuweze kubadilisha kanuni za ufanyaji biashara hii ili kuongeza tija katika uchumi wa nchi," alisema Dk. Gwamaka.

Mfanyabiashara wa vyuma chakavu, Robert Yohani, alisema mkutano huo umewapa matumaini makubwa ya kuendelea na biashara kwa kuwa waziri ametoa majibu mazuri kwa changamoto zilizopo na kuahidi kushughulikia kero mbalimbali.



Wanafunzi wa darasa la tano ambao walifanya mtihani wa darasa la nne mwaka jana wa Shule ya Msingi St Mary's Tabata, wakifurahia baada ya kutangaziwa matokeo mazuri ya darasa la nne kwa shule hiyo yaliyotolewa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sababu malalamiko ya mbegu feki kupungua

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MALALAMIKO ya wakulima kuhusu kupata mbegu feki za aina mbalimbali kwa mawakala ambazo hushindwa kuota shambani feki yamepungua kutoka 13 mwaka 2018/19 hadi kufikia 6 mwaka 2019/20.

Malalamiko hayo yamepungua kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI).

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, John Msemwa, alisema hayo jana kuwa malalamiko hayo yamepungua kufuatia elimu wanayoendelea kuitoa kwa wakulima kila wakati juu ya kuchukua risiti wanaponunua mbegu kwa mawakala na kutotupa vifungashio kabla mbegu hazijaota mashambani.

Alisema malalamiko hayo ya wakulima kutoka mikoa mbalimbali yamesababisha wakaguzi kutoka TOSCI kukagua sampuli za mbegu husika na walizobaini kutofanya vizuri shambani walizichukulia hatua ikiwamo kutoa amri ya kuziteketeza kwa moto chini ya usimamizi wa TOSCI.

Msemwa alisema, TOSCI inawahimiza wakulima kuendelea kutumia elimu wanayopewa, huku wakizingatia kupata na kutumia mbegu bora ili waweze kulima kilimo chenye tija na kupata mazao stahiki.

Naye Mkaguzi Mkuu wa Mbegu kutoka TOSCI, Emmanuel Mwakatobe, aliwaasa wakulima kuzingatia elimu wanayopewa ya kuhifadhi vifungashio na risiti baada ya manunuzi kwa mawakala na kuwasiliana na TOSCI wanapoona mazao waliyopanda hayajaota.

Alisema wakulima wanapaswa kununua mbegu kwenye maeneo husika ikiwamo kwenye maduka ya wauzaji wa pembejeo za kilimo ambayo yamesajiliwa badala ya minadani au kwenye magulio.

Mwakatobe alisema kwa mujibu wa sheria ya mbegu ya mwaka 2003 na maboresho yake ya mwaka 2014, imeweka utaratibu mzuri mkulima aliyenunua mbegu mahali sahihi akiwa na vithibitisho ikiwamo risiti na vifungashio, apate fidia ambapo TOSCI inaweza kumsaidia mkulima kupitia vyombo vya haki ikiwamo mahakama.

# Bashe ahamasisha uanzishaji mashamba makubwa alizeti

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewahamasisha viongozi wa mkoa wa Simiyu kuanzisha mashamba makubwa ya kilimo cha alizeti.

Bashe amesema Wizara ya Kilimo imedhamiria kutekeleza kauli ya Rais John Magufuli aliyoitoa wakati akizindua Bunge la 13 na kusisitiza umuhimu wa kuitumia Sekta ya Kilimo mazao kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania na kuwafanya Watanzania kuwa mabilionea.

Waziri Bashe amewaaambia viongozi wa mkoa wa Simiyu kuwa ili mkoa uwe na uwekezaji unaolipa, ni lazima kufikiria kutumia uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa njia ya uwekezaji katika mashamba makubwa, na kuiahidi wizara itatoa wataalamu kuanzia kwenye kufanya uchunguzi wa udongo kabla ya kuanza kwa uzalishaji na baadae utaalamu katika kilimo cha zao la alizeti.

Waziri Bashe amesema Mkoa wa Simiyu utapaa kimapato kutokana na uanzishwaji wa mashamba makubwa kwa kuwa ni rahisi kuendesha mashamba makubwa, ambapo ni rahisi kuwasaidia wakulima wakiwa katika eneo moja lakini pia ni rahisi kutoa utaalam na ushauri wa kuandaa mashamba, utoaji wa pembejeo bora na usimamizi.

"Ni rahisi kuwapa mikopo na teknolojia za kilimo na uvunaji kwa wakulima walio pamoja kuliko walio mbali," alisema.

"Ni rahisi kutumia teknolojia za uvunaji pamoja na uhifadhi, lakini kazi huwa ni rahisi kwa mnunuzi anapotaka kununua mzigo na kuuchukua kutoka kwa wakulima walio katika eneo moja."

"Naomba pia niwaeleze ni rahisi pia halmashauri zenu kukusanya tozo na ushuru mbalimbali kwa wakulima walio kwenye shamba la pamoja," alisema Bashe.

Aliongeza kuwa sekta ya kilimo mazao hususan kilimo cha alizeti ikitumika ipasavyo mkoa wa Simiyu unaweza kuongeza mapato ukilinganisha na sekta nyingine za kiuchumi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 19, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

Mawimbi bahari sasa chanzo kikuu nishati



Ukurasa 13

Unapolea mwenye mahitaji usiurejee ulemavu wake

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# INATISHA INAPODAIWA...

## ■ Walimu vinara wa ulevi na utoro, washirika wa ngono na wanafunzi

UALIMU ni taaluma mama inayozalisha wataalamu wote kama vile wanahabari, wahandisi, wahasibu, watawala, wasanii, madaktari, wachumi, marubani na wanasayansi.

Mafanikio ya taaluma nyingine zote hayawezi kutenganishwa na mchango wa mwalimu anayeshiriki katika utoaji wa maarifa, stadi na ujuzi, hatimaye kuzalisha wataalamu wengi wa kada mbalimbali ambao kwa pamoja huchangia maendeleo ya sekta zote kwenye jamii na taifa.

Mwalimu ni mdau muhimu katika taaluma ya ualimu kwani ndiye mtoaji wa maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali kwa wanafunzi wanaosomea taaluma na fani zote. Hivyo, mafanikio katika taaluma ya ualimu yanategemea sana mchango wake. Katika utendaji kazi, walimu wanaongozwa na maadili na miiko ya taaluma ili matarajio makubwa ambayo taifa linayo yaweze kutekelezwa kwa mafanikio na hatimaye nchi iweze kusonga mbele kimaendeleo kupitia mchango wa kukuza na kuendeleza ujuzi na maarifa.



Jukumu la mwalimu ni kukamilisha ufundishaji na usomaji siyo 'kuwakwaza kingono' wanafunzi hasa mabinti. **PICHA: MTANDAO.**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC) inayowajibika kusimamia nidhamu ya walimu nchini ili kudumisha maadili na uadilifu kwa walimu inapoanza mwaka ina ujumbe kwa walimu. Ni kutokana na ukweli kuwa pasipo nidhamu na maadili mema katika utendaji kazi, ni vigumu kutekeleza wajibu ipasavyo na hatimaye kupata matokeo chanya na ufanisi.

Mapema mwezi huu Kaimu Katibu wa TSC, Moses Chitama, akiwa katika mkutano na wanachama wa umoja wa walimu wakuu wa shule za msingi Tanzania Bara, anaibua makosa sugu yanayofanywa na baadhi ya walimu.

Anawapa wajumbe orodha ya madudu yanayoongoza kuripotiwa maeneo mbalimbali kuwa ni utoro, ulevi pamoja na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi. Chitama anasema: "Ninyi walimu msiposimamia maadili ya taaluma yenu pamoja na ya watoto mnaowafundisha tutakuwa na taifa bovu, lililokosa mwelekeo na lenye mmomonyoko wa maadili. Nawaambieni."

Utoro ni tatizo ambalo linakwamisha utoaji wa taaluma bora kwa wanafunzi. Mwalimu anaposhindwa kuhudhuria kazini kikamilifu, wanafunzi wanaathirika moja kwa moja kwani watashindwa kujifunza kutokana na kutokuwepo kwa mwalimu mwenye dhamana ya kuwapatia ufahamu na ujuzi kwenye somo husika iwe hesabu, lugha na sayansi.

Kwa kuwa tatizo la utoro kwa baadhi ya walimu linakwamisha jitihada za kuinua taaluma na maendeleo ya sekta ya elimu, mwaka 2021 anashauri uwe mwaka wa kuanza ukurasa mpya kwa walimu kwa kuhakikisha kuwa wanahudhuria kazini kama inavyotakiwa na kufundisha kama ilivyo wajibu wao ili wanafunzi wapate maarifa stahiki wanayopaswa kuyapata shuleni kwa wakati na kwa mujibu wa maelekezo ya mitaala.

Aidha, anawashauri walimu wathamini kazi yao kwa kukumbuka kuwa taifa lina imani nao katika utoaji wa elimu na hivyo wana wajibu wa kuhudhuria kazini kama taratibu za kazi zinavyotaka. Na pale panapokuwapo na sababu ya msingi ya mwalimu kushindwa kufika kazini, basi atoe taarifa kwa mkuu wake wa kituo cha kazi ili asihesabike kuwa ni mtoro.

Suala la ulevi kwa baadhi ya walimu linatajwa kuwa ni kikwazo cha ufanisi wa taaluma ya ualimu. Ni wakati muafaka kwa baadhi ya walimu wanaotumia kilevi kujitathmini kwa kuhakikisha kuwa unywaji wao wa pombe hauathiri jukumu la ufundishaji walilonalo. Kama mwalimu atakunywa kupitiliza hadi kufikia kwenda kazini akiwa amelewa au kunywa pombe muda wa kazi, ni dhahiri ufanisi wa kazi hautakuwapo na hivyo kuathiri utoaji wa taaluma kwa wanafunzi wake.

Vilevile, ukosefu wa maadili na kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi kwa baadhi wa walimu na wanafunzi unatajwa kuwa inashusha heshima waliyonayo walimu kwa jamii na taaluma ya ualimu kwa ujumla.

Walimu wanategemewa na serikali, jamii, wazazi, walezi na wananchi kuwa walezi bora kwa wanafunzi wao kutokana na jukumu la kimalezi walilonalo walimu.

Kwahiyo, walimu wanategemewa kuwalea vyema wanafunzi wao katika misingi ya malezi ya kifamilia ambapo mwalimu ni baba au mama na mwanafunzi ni mtoto.

Katika mazingira haya, mwalimu hategemewi kuwa chanzo cha kumrubuni mwanafunzi wake kwa kuanzisha uhusiano wa mapenzi.

Kutokana na wajibu wa kimalezi walionao walimu kwa wanafunzi wao, ni vyema walimu wakajiepusha na tabia ya uhusiano na wanafunzi wao ili kuendeleza sifa na heshima waliyonayo walimu katika jamii na taifa.

Uhusiano wa kimapenzi unasababisha mwalimu aliyethibitika katika jambo hilo kufukuzwa kazi na mwishowe kufungwa jela miaka 30, iwapo anapatikana na hatia ya ubakaji na unyanyasaji mwanafunzi au mtoto huyo.

Walimu wakumbuke kuwa wajibu walionao wa kulitumikia taifa ni kufanikisha wanafunzi kusoma na kufanikiwa kitaaluma kwa vile elimu ndiyo moyo wa taifa na endapo walimu watatimiza wajibu wao, huku wakizingatia nidhamu, maadili na miiko ya kazi katika utendaji kazi wao wa kila siku, taifa litasonga mbele kimaendeleo pengine kwa haraka zaidi.

Naamini 2021 utakuwa mwaka wenye mabadiliko kwa walimu kujisahihisha katika makosa sugu ambayo TSC imeyaorodhesha ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi na hatimaye uwekezaji mkubwa unaofanywa katika sekta ya elimu uweze kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa maendeleo endelevu.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko Kongwa Mkoa wa Dodoma. Maoni: 0765-409249.***

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Uwekezaji kwenye vipaji utakavyochochea kujiajiri



Ubunifu na vipaji unaoonekana kwa kazi hizi za Tinga Tinga ni miongoni mwa vipaji vya kipekee nchini. Kukuza vipaji na kuwawezesha vijana shuleni ni moja ya maeneo yanayoweza kuchochea ujasiriamali na kujiajiri. **PICHA: MTANDAO.**

ZIKO dalili kuwa licha ya kiwango cha kufaulu darasa la saba kuwa kikubwa na elimu ya sekondari kuenea kote, kuna walakini wa hatua zinazofuata hasa kuwezesha vijana hao wasomi kuwa na ujuzi na kujiajiri.

Jitihada za kuingiza dhana ya kujiajiri ipo katika suala la ujasiriamali zaidi, ambao unachukuliwa kama kuanzisha biashara fulani, wakati kinachohitajiwa ni kutumia vipaji katika eneo hilo ili kuwa mbunifu na mtafutaji.

Cha msingi kiwe ni umuhimu wa kutumia vipaji, au kuvijenga wanafunzi wakiwa bado shuleni.

Hisia ya kuwapo kwa mwelekeo tofauti licha ya kuwa ni kama kuashiria kuwa kuna jambo linaweza kufanyika zilionekana mwishoni mwa mwaka jana katika maelekezo ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako, akizungumza na maofisa wa elimu wa mikoa na wilaya. Alitilia mkazo umuhimu wa maofisa elimu kuhakikisha kuwa kila kada ya elimu inafanyiwa kazi jinsi inavyopasa, ikiwa ni pamoja na michezo, kilimo na elimu maalum (hasa kwa wanaoishi na ulemavu. Licha ya kutotaja maeneo mengine ya kada za elimu, bado mkazo huo unaelekea ulilenga vipaji vya nje ya madarasa.

Ukichukulia kwa upana, unaweza kuangalia wakati elimu ilipokuwa inatolewa hadi darasa la nane kama shule ya msingi (kuanzia darasa la tano ilikuwa inaitwa shule ya kati) kabla ya kubadilishwa na kuwa miaka saba ya sasa. Moja ya maeneo yaliyopunguzwa ni stadi za ufundi seremala na vifaa vyake, michezo kama darasa, au kujifunza maigizo, kilimo ambacho baadaye kilianza kuonekana kama ni uzalishaji halisi badala ya shambadarasa kujua zaidi kuhusu mazao, maji, udongo na viuatilifu. Kimsingi elimu ya vitendo na vipaji ilipauka kwa haraka.

Bado hakuna uhakika kuwa wizara inataka kurudisha upana huo wa elimu, lakini endapo suala ni kukuza vipaji badala ya ufahamu wa maarifa katika vitabu na kujiandaa kusoma zaidi au kujua kusoma na kuandika ili kuwa mwananchi wa kawaida, yako mengi zaidi ya kufanya. Jambo la kushangaza ni kuwa wakati elimu hii ya vipaji inawekewa kipaumbele, kazi za ofisini na kwingineko za ajira ya moja kwa moja zilikuwa zinapatikana kwa urahisi.

Hata ngazi ya darasa la nane walikuwa wanapata ushauri ni wapi mwanafunzi anataka kwenda anapohitimu; wakati baada ya sekondari nafasi zilikuwa hazina taabu, lakini hali ilibadilika zikapungua hatua kwa hatua na sasa zimeondoka.

Katika miaka ya karibuni, ushauri wa wapi mwanafunzi anataka kwenda baada ya kuhitimu hata kwa vyuo vikuu labda hauhitajiki sana kwani kazi ni za kubahatisha na pengine ni katika ngazi ya uzamili au stashahada baada ya shahada ndiyo angalau anaweza kuhisi labda anakubalika bila taabu maeneo tofauti.

Huwezi kusema kazi hazipo kwa wenye vyeti, stashahada au shahada ila mara nyingi ni za kubahatisha, ingawa si haba kupita kiasi, ina maana elimu inayolenga vipaji inahitajiwa zaidi wakati huu kuliko mwanzoni na hivyo siyo ajabu suala hilo likaanza kueleweka sasa.

> Huwezi kusema kazi hazipo kwa wenye vyeti, stashahada au shahada ila mara nyingi ni za kubahatisha, ingawa si haba kupita kiasi, ina maana elimu inayolenga vipaji inahitajiwa zaidi wakati huu kuliko mwanzoni na hivyo siyo ajabu suala hilo likaanza kueleweka sasa.

Yako maeneo mengine yanayochochea kuzingatia suala la vipaji kupitia elimu pana zaidi shule za msingi na sekondari.

Kimsingi elimu ya sekondari hivi sasa ni nyongeza tu kwa ile msingi, kwani maeneo mengi ambayo kinadharia yanafundishwa msingi hata sekondari hawayaelewi, kwa mfano 'irregular verbs' kufundishwa darasa la tatu.

Ni mifumo tatanishi ambayo inatoa picha ya mafunzo au masomo ya hali ya juu, bila mazingira halisi ya kujikita katika hisia au akili ya mtoto au unaweza kusema ni upungufu wa ustahimilivu (resilience) kimasomo.

Tatizo la kuongeza masomo ya kivipaji kwa mfano michezo, maigizo, sarakasi, useremala, kilimo na uchongaji (kuna wakati kulikuwa na somo la lishe au mapishi).

Wanafunzi walijifunza maarifa ya nyumbani kama kufua, kupika, kushona na kudarizi na kuwa uratibu wake kwa uwiano na masomo mengine.

Kinacholeta tatizo hapo siyo elimu ambayo mtoto atakuwa amepata au amekosa kwa mfumo kubadilishwa, ila utaratibu wa mitihani na vyeti, tatizo la kirasimu na sio la kimaisha, lakini linaweza kuvuruga urekebishaji wa mifumo inayohusika. Wataalamu hawatakubaliana vigezo na vipaumbele mwanafunzi au mtoto anahitaji nini kwa lazima, au achague mwenyewe kivipi?

Kinachoonekana kwa haraka ni kuwa masomo-mafunzo yanahitaji msingi mpana ili aina tofauti za vipaji vya watoto ziibuliwe wakiwa wachanga na zikianza kuonekana, kama ni za lugha, ushairi, michezo, maigizo au ubunifu wa kisanyansi.

Hili lifanyike badala ya ule mkazo (hasa enzi za ujamaa) kuwa kila mwanafunzi lazima asome sayansi, baadhi yao walipata shida kutoka kidato cha tatu kwenda cha nne baada ya kuona masomo ya sayansi ni usumbufu, hayaeleweki na kujitahidi kuendana na anachofundisha mwalimu (hasa hesabu na fizikia).

Ilikuwa ni kurudisha nyuma kujisomea masomo yenye kuleta matumaini hasa ya kuingia kidato cha tano, yaani katika fani za Sanaa (lugha, historia, jiografia na fasihi) au biashara.

Licha ya kuwa siyo rahisi kufanya utabiri katika hali ya sasa, inavyoelekea elimu halisi ya msingi ni kuanzia darasa la awali hadi la nne ikibidi, halafu baadaye kuwe na elimu mafunzo kwa mikondo ya vipaji.

Msingi wake ni kuwapo kwa maeneo mapana ya nyanja za stadi za ufundi, jamii, sayansi, sanaa, michezo, kilimo na biashara hali inayofanya elimu ya kati yaani miaka mitatu ya ziada ya shule ya msingi na ile minne ya sekondari iwe ni kitu kimoja. Halafu kuwe na elimu ya ngazi ya juu inayochukua muda mrefu zaidi vyuoni.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Unapolea mwenye mahitaji usiurejee ulemavu wake

UJUMUISHI wa watu wanaoishi na ulemavu kwenye elimu na mambo mengi ya kijamii ni eneo linalosisitizwa na serikali ili kusiwapo na ubaguzi wala anayeachwa nyuma katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo, kielimu, kiuchumi hata kisiasa.

Hatua hiyo inachukuliwa kwa sababu ulemavu wa viungo si tatizo, hivyo wanachohitaji watu wanaoishi na ulemavu, ni kupatiwa fursa, njia mbadala na kupewa mbinu za kujitegemea.

Ujumuishi unakumbusha wazazi na jamii kuwakubali wenye ulemavu kuwa ni binadamu wa kawaida na kwamba ulemavu ni upungufu kwenye viungo na kwamba wanabaki kuwa watu waliokamilika kama walivyo wengine, ni kwa mujibu wa Peter Kisanga.

Kisanga kutoka kitengo cha kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Shule Kuu ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anaeleza katika mahojiano na Nipashe kuhusu elimu jumuishi na namna ya kumlea mwenye ulemavu ili akue na awe kama raia wengine.

Anasema cha kwanza mzazi au wazazi wanapopata mtoto anayeishi na ulemavu wajikubali wao kwanza pamoja na mtoto. Wafahamu kuwa ni upungufu kwenye viungo mfano haoni, hasikii au ana ualbino na kumtafutia namna bora ya kukua na kumudu maisha yake.

"Kama haoni asaidiwe kwa kupewa miwani, fimbo nyeupe ili atembee, maandishi ya nukta nundu ili asome. Kama hana mikono atumie miguu kula na kuandika."

Kisanga anawaambia wazazi wakubali na waache kulaumiana hasa kuwasingizia wenza (wanawake) kuwa wanahusika na kupatikana mtoto mwenye hali ya ulemavu.

"Kama umepata mtoto mwenye ualbino fahamu baba na mama mnahusika, wote mna nasaba zenye ualbino. Usimsingizie mwenza wako kubalini kuwa wote mna mchango na kuacha kulaumiana," anakumbusha.



Watoto waelekezwe bila kuonyeshwa tofauti zao. Wote wapewe haki na mahitaji sawa kuepusha ubaguzi na unyanyapaa. **PICHA: MTANDAO**

**KUOMBA MSAADA**

"Inawezekana umekwama hujaweza kumkubali mtoto wako na moyo ni mzito. Nenda ofisi za ustawi wa jamii, wasiliana na vyama vinavyohusika na kuhudumia watu wenye mahitaji maalumu mfano Chama cha Wenye Ualbino (TASS), Under the Same Sun (UTTS) au Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) eleza shida yako."

Kisanga ambaye ni mwalimu wa wenye mahitaji maalumu, anaonya tabia ya kwenda kwa waganga, kufikiria kutalikiana, kutelekeza au kuwadhuru watoto kisa ni wana ulemavu akisema ni mambo ya kukwepa.

**UANZE UWAJIBIKAJI**

Mwalimu Kisanga anakumbusha kuwa serikali inatoa fungu la utambuzi wa watu wenye changamoto au mahitaji maalumu hivyo ni wakati wa idara ya ustawi wa jamii kulitumia na kuwatambua watoto wenye uhitaji na kuwasaidia.

Anasema kama kijijini amezaliwa mtoto mwenye ualbino akizaliwa wazazi wake wanaweza kuelimishwa na kuhamasishwa kufahamu hali hiyo ili kumkubali na kumsaidia.

"Hata taasisi za kuhudumia wenye ulemavu kama TAS, UTSS na SHIVYAWATA na vyombo vya habari zikiwamo redio za jamii zinawajibika kushuka chini na kuwafikia wenye uhitaji ili kuwasaidia kwa vile siyo rahisi mzazi au mlezi akasafiri kutoka kijijini kufuata mashirika hayo mijini au kuviendea vyumba vya habari. Kwanza hawana uwezo, hawazifahamu na wapo wengine waliokata tamaa."

Anashauri kuweka miundombinu ya utambuzi ya kuwafuatilia na kuwafikia iwe kijijini, vitongoji au mitaa kupitia viongozi wa serikali wa maeneo hayo ambao wana taarifa za idadi ya familia, wakazi na watoto wanaozaliwa.

**WAKATI WA MALEZI**

Lucy Msafiri, kama alivyo Kisanga, anawahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Shule Kuu ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anapozungumzia kulea watoto wenye mahitaji maalumu ili kuwapa nafasi ya kunufaika na elimu jumuishi anasema:

"Unapomlea mtoto pengine mwenye ualbino usimwambie wewe una kasoro au tatizo hili. Hapana. Usifanye hivyo. Mzazi au mlezi daima mwambie mtoto wewe ni binadamu kama walivyo wengine. Umsaidie kutatua shida yake. Kama ana uoni hafifu mpatie miwani.Mpe mafuta ya kupaka ngozi yake na mavazi ya kumkinga na mionzi ya jua."

Anasema penda kumsifu mtoto wako na usimwonyeshe kuwa ana tofauti, kwa mfano usimtenge afanye kazi kama wengine. Aoshe vyombo, afue nguo zake, apike chakula.

Wahimize wote kunywa maji ili kulinda ngozi ya mwenye ualbino, wape lishe bora yenye matunda na mboga kwa wingi, walishe wote chakula cha nafaka zisizokobolewa kuanzia dona, unga wa ngano usiokobolewa, samaki, dagaa na vyakula vya protini, wote bila kumbagua anayeishi na ualbino.

Anashauri wote walishwe vyakula vyenye vitamin A kama karoti, viazi vitamu, spinach, njegere kwa vile vinaongeza rangi kwenye ngozi na ni njia ya kuimarisha afya ya mwenye ualbino. Mara nyingi wahimizwe kuvaa viatu na kuepuka kwenda maeneo yanayoweza kuwaumiza ngozi, iwe kwa watoto wote.

"Anapouliza mbona mimi niko hivi au sina hiki jibu lako liwe wewe ni binadamu wa kawaida. Unafikiri kama wengine. Unalala na kuamka. Wewe ni wa kawaida, hakuna tatizo. Ngozi yako imekuwa na upungufu wa rangi ya asili, lakini si tatizo wewe ni kama watu wengine wote."

Anawashauri wazazi kuwafundisha watoto kujikubali kuwa ni binadamu kama wengine, wanasoma, wanakua, ni viongozi, wachungaji na hakuna cha kuwazuia kuishi maisha yao.

"Epuka kusema eti wewe ni mlemavu na kumtenga, achana na mambo hayo. Ukiwapeleka watoto kwenye ibada nenda nao wote. Kwa vile mwenye ualbino hashauriwi kutembea wakati wa jua kali wazuie watoto wote, kutembea juani wala kufanyakazi wakati wa jua kali."

Lucy, anawataka wazazi na walezi kuacha kauli za taharuki na kuwafokea watoto wakirejea hali zao za ulemavu, kwa mfano; "Wewe unajua una ualbino kwanini unatembea usiku ukishambuliwa?"

Anashauri kuwa wazazi wawapangie muda watoto wote bila kumtenga anayeishi na ualbino kuwa wanatakiwa kurudi nyumbani saa flani pengine, saa 10 jioni na ni marufuku kwa yeyote kurudi nyumbani usiku. Wote wafuate utaratibu na kusiwe na utofauti. Na akikosea aonywe au kuadhibiwa.

Anasema kutomtenga mtoto na kuachana na kumwonyesha kuwa ni wa tofauti kunamjengea kujiamini, kujikubali na kuwa madhubuti na kujibu vijembe, kejeli au unyanyapaa wowote, anaokutana nao kwa vile amefunzwa kujiamini, kujitambua na kujikubali.

**ANGALIZO KWA BINTI**

Lucy anasema ni vyema mama kumweleza binti anayeishi na ulemavu wowote, mathalani ualbino ukweli wa mambo ya kupevuka, hadaa za ngono kwa mabinti na kumfahamisha namna ya kujibu pale anapokutana nazo.

"Mweleze binti kuhusu mabadiliko ya mwili wake na kupevuka. Na kila kitu kitakachotokea. Umfundishe na afahamu. Mwambie pia kuhusu kujamiiana kwamba anapohadaiwa atoe majibu gani kwa wanaomdanganya. Mfano akiambiwa nakupenda anaweza kujibu 'hunipendi unachotaka ni ngono na kunidhalilisha. Niache." Akiambiwa nataka nikuoe ajibu 'hakuna ndoa wala mapenzi kwa binti anayesoma', huwezi kumuoa mwanafunzi acha uongo'. Nitatoa taarifa kwa mwalimu, wazai na polisi kuwa unanihadaa ili ushitakiwe.'

**KUBADILISHA MITIZAMO**

Akizungumzia changamoto zinazowakabili wanaoishi na ualbino Ofisa Ugharibishaji wa Taasisi ya Under the Same Sun, inayoshughulikia ustawi wa wenye ualbino, Seif Kondo, anasema mara nyingi, wenye ualbino wanakuwa na simanzi na kusononeka.

Anasema ni kutokana na kukataliwa na wazazi na jamaa zao, kuachwa vijijini kulelewa na bibi au babu zao, wakati mwingine kuchekwa iwe darasani, au kwenye jamii,kunyanyapaliwa na kupewa majina ya kejeli kama 'zeruzeru au zungu au china'.

Jingine analotaja Kondo ni pamoja na wanaoishi na ualbino wengi kukosa matunda ya elimu kama kusoma na kuelimika, kupata kazi na kuwa na haki za kijamii. Yote hayo yanawafanya wasononeke na kujiona kuwa wana bahati mbaya.

Hata hivyo, wazazi na walezi wakiwapenda, kuwajengea kujiamini na kujikubali kuwa ni binadamu wa kawaida, walimu darasani nao wakawapa kipaumbele na kuwasaidia kujifunza na kukuza vipaji vyao wanamudu maisha yao, wasiwe na sononа wala kuwa tegemezi kwenye jamii, anasema Kondo.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# Mawimbi bahari sasa chanzo kikuu nishati

## ■Uingereza, Italia wayatumia kuvuna umeme



Pichani ni mapanga boi yanayokusanya na kuchakata mawimbi kupata umeme. **PICHA: ZOTE MTANDAO**

WAKATI wengi wanakimbilia ufukweni kubarizi na kupunga upepo unaovuma kutoka kwenye mawimbi makubwa kwa madogo ya bahari, wavumbuzi na watafiti wa nishati jadidifu wanapofika ufuoni hawabarizi tu, hupasua vichwa na kubuni mbinu za kuyatumia mawimbi bahari kuzalisha nishati.

Kinara wa ugunduzi wa nishati ya mawimbi bahari anayejizoelea sifa nyingi wakati huu ni Yoshio Masuda, kutoka Japan, akiwa komandoo wa jeshi la majini, Masuda, ameibua vyanzo vingi vya nishati hiyo na kuvitumia kwenye vyombo vya usafiri majini na kuwasha taa pia.

Anaeleza kuwa nishati ya mawimbi ya baharini, ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya nishati jadidifu (renewable) ambavyo havina mwisho kama ilivyo umeme jua na upepo na kwamba bila shaka itaendelea kufungua ukurasa mpya wa kupatikana kwa umeme wa kutosha na endelevu wa kuendesha mitambo ya uzalishaji, utoaji huduma pamoja na matumzi ya nyumbani.

'Wave energy' kama inavyofahamika kitaalamu, ni nishati inayopatikana kutoka kwenye mawimbi ya bahari ambayo yakiwekewa vifaa na mitambo ya kuyachakata kama transfoma yanazalisha umeme unaotumika nyumbani, viwandani, kuondoa chumvi majini na kuendesha vyombo vya usafiri zikiwamo meli, mashua na majahazi.

> “Kazi hiyo si kwa shule za sekondari tu bali za msingi na shikizi (awali), wamejitolea nguvukazi na fedha pia, lengo likiwa ni kuhakikisha kila shule inakuwa na miundombinu inayohitajika,” anasema na kuongeza kuwa anaamini ujenzi wa madarasa utakamilika hivyo wanafunzi

Kazi ya Masuda ni mwendelezo wa utafiti katika sekta hiyo ulioanza tangu miaka ya 1970, wakati wa uhaba wa mafuta duniani ulitikisa kuanzia mwaka 1973 kutokana na Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu Zinazosafirisha Petroli (OAPEC) kuweka zuio la usafirishaji mafuta, ukawa mwanzo wa kusaka nishati mbadala.

Hata sasa 'wave energy' haijatumiwa na nchi nyingi duniani licha ya kwamba ni inaonekana ni chanzo cha nishati kipya, lakini baadhi ya mataifa hajaweza kunufaika na mawimbi bahari. Ziko nchi kadhaa ambazo zimeanzisha mashamba ya umeme wa mawimbi bahari (wave farms) nazo ni pamoja na Ureno, Uingereza, Australia na Marekani.

Ureno ilikuwa na shamba la umeme wa mawimbi lililopewa jina la Aguçadoura lililokuwa jirani na jiji la Porto lililowekewa mitambo ya kuchakata mawimbi kuzalisha umeme na kwa kuanza zililengwa kupatikana megewati 2.25 na kuanza kazi 2008, lakini haijafanyakazi kutokana na changamoto za kiuchumi.

Kwa Uingereza kuanzia mwaka 2010 shamba la umeme wa mawimbi lilianzishwa Scotland na mwaka 2007 ilitangazwa kuwa uzalishaji wake ungegharimu zaidi ya paundi milioni milioni.

Uingereza katika pwani ya Cornwall ilianzisha shamba la umeme bahari lililokuwa lizalishe megawati 20 lakini pia likilenga zifikie megawati 40 na kwa wakati huo lilitarajiwa kuunganisha wateja au kaya 7,500 na kusaidia kudhibiti tani 300,000 za hewa ukaa kwa miaka 25 ijayo. Mashamba hayo yanapatikana Marekani, Russia na Italia.

### FAIDA UMEME BAHARI

Mawimbi ni mengi kama ambavyo dunia imezungukwa na bahari kwa kiwango cha asilimia 71 na bahari kubwa zaidi ni Pacific, zipo nyingine kadhaa ikiwamo Mediterranean Indian na Atlantic. Wingi wa bahari hizo unaamaanisha wingi wa mawimbi duniani.

Faida lukuki za umeme huo ni pamoja na ukweli kuwa ni nishati isiyochafua mazingira wala kuumiza utando wa tabaka la ozone ambalo linamomonyoka kutokana na ongezeko la hewa ukaa duniani linalosababisha joto kali na mabadiliko ya tabianchi. Nishati zinazoongeza joto duniani ni za visukuku (fossils) ambayo ni mabaki ya viumbe hai kama wanyama na mimea yaliyofunikwa ardhini kwa muda mrefu na kutengeneza gesi au mafuta.

Nishati ya mawimbi ya bahari ni jadidifu (renewable) haimaliziki ni kama ya upepo na jua ni vitu visivyomalizika mpaka mwisho wa ulimwengu na mawimbi yamejaa muda wote baharini na kila wimbi linaloonekana linaweza kutumika kuzalisha umeme bila kujali ni makubwa au madogo. Kwa wingi huo umeme wa mawimbi ni kudumu si kama wa maji ambao maporomoka yake yanatishiwa na ukame unaotokana na mabadiliko ya tabianchi au joto jingi linaloumiza uoto wa asili.

### HOFU KIUWEKEZAJI

Uwekezaji ndani ya bahari unaweza kuwa na athari kwa mazingira na viumbe bahari na unaweza kuubadili muonekano wa bahari. Inaweza kuwa chanzo cha kukwamisha utalii hasa wa baharini na visiwani .

Kuna wasiwasi kuwa umeme wa bahari unaweza kuhatarisha maisha ya viumbe wa baharini na kuvuruga ekolojia kwa sababu miundombinu yake inawekwa kwenye maeneo ambayo huenda pia ani mazalia na makazi ya viumbe wa majini hasa sehemu zenye kina ambacho kina mawimbi makubwa.

Eneo jingine ni gharama kubwa za kuweka miundombinu ya umeme bahari kwa vile vifaa na mitambo yake ni ghali zaidi na inahitaji teknolojia ya hali ya juu kuanzia uundwaji, uwekaji na uvunaji wa umeme huo.Lakini, pia kuna ukarabati na ufungaji upya kila wakati inapodi kutokana na bahari kujaa chumvi.



# TAKUKURU kusikiliza madai rushwa TANESCO

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, inatarajia kuanza kusikiliza kero za rushwa zinazotokana na kuunganisha umeme ili kukomesha vitendo hivyo kwa wananchi.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa wataanza kusikiliza kero hizo kuanzia Februari Mosi hadi Machi, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali jijini hapa.

Kibwengo alisema wananchi wanapaswa kuitumia fursa hiyo vizuri kutoa kero mbalimbali za rushwa kwa taasisi hizo ili kuwapatia ufumbuzi.

**Pamoja na hayo tumejipanga kukutana na wananchi kila Jumanne ya kwanza ya mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero mbalimbali.**

"Tutakuwa na programu ya kukutana na wananchi katika maeneo tofauti, tunaomba wajitokeze kwa wingi kutumia fursa hiyo kutoa kero zao," alisema Kibwengo.

Alisema taasisi hiyo itakusanya kero hizo na kuzichunguza ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika.

"Pamoja na hayo tumejipanga kukutana na wananchi kila Jumanne ya kwanza ya mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero mbalimbali," alisema.

Pia alisema katika ufuatiliaji wao wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kuhamasisha ushiriki wa wadau na wananchi katika mapambano ya rushwa ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuelimisha jamii.

Alisema katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka jana, wameendesha semina 75, maonyesho 11 na mikutano 49 ya hadhara ya kuelimisha mapambano dhidi ya rushwa ambayo yameleta matokeo chanya kwa taasisi hiyo.

"Semina na maonyesho katika mihadhara imesaidia sana kuwapa uelewa wananchi. Hivi sasa wengi wao wanaelewa nini maana ya rushwa na kutoa taarifa pale wanapoona sehemu kuna viashiria vya rushwa," alisema Kibwengo.

Pia alisema mapambano dhidi ya rushwa wameimarisha ambapo zipo klabu 165 za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo mkoani hapa ambazo hutumika kutoa elimu kwa wanafunzi.

Alisema klabu hizo kwa kushirikiana na TAKUKURU wamekuwa wakisaidia kutoa elimu kwa jamii namna ya kupambana na rushwa kwa kuwaelimisha kujua haki yako ya msingi.

## Wataka vifaa uokozi majini

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAKAZI wa vijiji vilivyoko jirani na Bwawa la Mtera wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wamewaomba wamiliki wa vyombo vya usafirishaji wa majini kuweka vifaa vya kujiokoa ili kulinda maisha yao wanapotumia usafiri huo.

Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walisema vyombo vinavyotumika katika bwawa hilo ni boti na mtumbwi ambavyo husaidia kutoa huduma ya usafiri kwa kuwavusha eneo la pili la bwawa, lakini havina vifaa vya kujiokoa kipindi inapotokea ajali majini.

Mmoja wa wananchi hao, Mkazi wa Kijiji cha Igunguli, Halima Athumani, alisema hulazimika kupiga mbizi pindi inapotokea boti au mtumbwi umepata ajali au kuharibika kabla ya kufika eneo husika.

"Kitendo hicho kwa kweli kinahatarisha maisha yetu. Vyombo hivi vya majini havina vifaa vya kulinda usalama wa abiria, hakuna majaketi wala maboya kwa ajili ya kuogelea endapo imetokea ajali," alisema.

Naye mkazi wa kijiji cha Loje anayejishughulisha na uvuvi, Komba Ngonyaji, alisema wamelazimika kuomba vifaa ili kulinda usalama wao.

"Bwawa la Mtera kuna viboko wengi wakati mwingine ikitokea mtumbwi umepinduka na kusababisha abiria kuzama wanaweza kupoteza maisha, lakini tukiwa na vifaa itarahisisha kujiokoa kwa kuogelea na kupata msaada wa waokoaji kwa urahisi," alisema.

Mmiliki wa boti anayetoa huduma ya usafiri kwenye bwawa hilo, John Mapunda, alikiri kwa vifaa hivyo licha ya kutoa huduma ya usafiri kwa muda mrefu.

"Kwa miaka mingi tumekuwa tukiwasafirisha wakazi waishio kandokando na bwawa hilo la Mtera kwenye shughuli zao mbalimbali ikiwamo za uvuvi na kilimo," alisema.

Hata hivyo, aliwatoa hofu wananchi hao kwa kuwa watajitahidi kutafuta vifaa hivyo.

Diwani wa Viti Maalum, Hilda Kadunda, alisema ni wajibu wa mamlaka zinazosimamia vyombo hivyo kuchukua tahadhari kabla ya kutokea ajali ili kuwapo na vifaa vya kujiokoa. Alisema wamiliki hao wamekuwa wakiwasafirisha abiria hao kwa nyakati zote ikiwamo usiku na mchana huku wakiwa hawana vifaa hivyo.



Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi (kushoto), akikagua miundombinu ya daraja linalounganisha Kijiji cha Gwandi na Zajilwa Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, mwisho wa wiki kwenye ziara yake ya kutembelea jimbo hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge atoa mifuko 430 ya saruji ujenzi wa madarasa

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

MBUNGE wa Chamwino, Deogratius Ndejembi, ametoa mifuko ya saruji 430 ili kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye baadhi ya shule zilizoko jimboni hapa ili wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza waanze masomo.

Ndejembi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, alitoa mifuko hiyo katika ziara aliyoifanya katika kata za Haneti, Zajilwa na Itiso na kubaini baadhi ya vyumba vya madarasa havijakamilika ujenzi.

Alisema ametoa mifuko hiyo pamoja na Sh. milioni 15 kwa kata hizo ili zikamilishe ujenzi wa vyumba hivyo vitakavyotumiwa na wanafunzi hao.

"Wananchi, ubunge huu nilio nao ni mali yenu. Hata mshahara ninaopata ni wenu, hivyo siwezi kuona watoto wetu wanakosa masomo na mimi nikanyamaza. Nimeona nifike ili tushirikiane kukamilisha vyumba hivi vya madarasa ili watoto wetu wote waanze masomo," alisema.

Mbunge huyo aliwahakikishia wananchi kuwa ataendelea kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi kila shule jimboni humo, ili kuwaondolea kero zinazowakabili.

Akiwa katika ziara hiyo, Kata ya Zajilwa, Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Gefile Tamba, alisema kata hiyo haina shule ya sekondari ambapo watoto hulazimika kutembea umbali wa kilomita zaidi ya 16 kufuata masomo Shule ya Sekondari Segala.

Alisema kutokana na tatizo hilo wameanzisha michango kwa ajili ya ujenzi wa shule ya kata yao, ili kuhakikisha inaanza kutoa huduma ya masomo mwaka ujao.

Alibainisha kuwa sekondari hiyo itakayojengwa itawahudumia watoto kutoka vijiji vya Magungu, Zajilwa na Gwandi ambapo kwa sasa wanatumia Sekondari ya Segala.





## Hemed ageukia uwekezaji elimu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wazee na wazazi kuendelea kuwekeza katika sekta ya elimu ili jitihada hizo ziwe fursa na matunda bora yatakayowajengea njia sahihi watoto katika maisha yao.

Hemed aliyasema hayo jana kwenye Mahafali ya Nane ya Chuo cha Afya Zanzibar waliotunukiwa stashahada katika fani za uuguzi na ukunga, ushauri masihi, ofisa tiba pamoja na astashahada ya ushauri nasihi, hafla hiyo ilifanyika katika uwanja wa michezo wa Mao Zedong.

Alisema umefika wakati wazazi na wazee lazima wabadilike na kujenga utamaduni wa kutumia nguvu zao katika elimu badala ya kuendeleza tabia ya kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kuwafanyia sherehe wakati wanapofunga ndoa.

Makamu huyo wa Pili wa Rais alibainisha wazi kwamba elimu pekee katika karne hii ya sayansi na teknolojia, ndiyo itakayowawezesha watoto kuingia katika ushindani na watoto wenzao duniani katika mfumo wa kujiamini kwenye soko la ajira.

Aliwapongeza wahitimu hao kwa kukamilisha mafunzo yao, lakini wanalazimika kujipanga upya kwa kazi iliyo mbele yao namna watakavyolihudumia taifa katika misingi ya uaminifu na uadilifu kama walivyokula kiapo kwa wale wa kada ya uuguzi na ukunga.

Pia aliwaasa wahitimu hao katika hatari ya kuachwa nyuma kielimu baada ya miaka michache ijayo endapo hawatakuwa tayari kujielimisha zaidi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Hemed pia aliupongeza Uongozi wa Chuo cha Elimu ya Juu katika Kada ya Afya ya Zanzibar kwa kuanzisha mafunzo ya fani ya dawa yaliyotanguliwa na yale ya kukabiliana na majanga ambayo wataalamu wake bado ni wachache.

Aliutaka uongozi wa chuo kujipanga katika mwelekeo wa malengo yake ya kuelekea kuwa chuo kikuu na akaahidi kwamba serikali iko tayari kuunga mkono malengo hayo.

# Wataka sheria kurekebishwa kufikia uchumi bluu wa uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wavuvi wa Kojani Zanzibar (KOFDO) imetaka kufanyiwa marekebisho Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2010 ili kufikia uchumi wa buluu wa uvuvi.

Akizungumza katika mkutano wa jumuiya hiyo uliofanyika katika Shule ya Kisiwandui, Mwenyekiti wa KOFDO, Omar Mohamed Ali, alisema sekta ya uvuvi inakabiliwa na vikwazo vingi ikiwamo upungufu wa sheria ya uvuvi ya mwaka 2010

Alisema sheria hiyo ina upungufu ambao unawakandamiza wavuvi vikiwamo vifungu vya 17 na 21(1) vya sheria hiyo na kama upungufu huo hautafanyiwa marekebisho utarudisha nyuma juhudi za uchumi wa buluu kwa sababu kutakuwa hakuna utulivu baharini.

Alisema uchumi wa buluu umebeba mambo mingi ikiwamo biashara, utalii na uvuvi na dhamira ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuifanya Zanzibar ya kibiashara ili kutoa mirija ya kifedha ambayo itainua uchumi wa taifa.

**Tangu kutangazwa kwa sera ya uchumi wa buluu, idadi ya watalii Zanzibar imeongezeka na uchumi umeanza kukua.**

"Ajira nyingi zinatokea kutokana na uwekezaji wa kibiashara, hivyo ni vyema sekta za biashara, utalii na uvuvi kukuzwa na kuendelezwa kwa sekta hiyo. Sisi jumuiya ya wavuvi wa Kojani tuko tayari kuiunga mkono serikali katika kuinua uchumi wa nchi kupitia uvuvi," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema tangu kutangazwa kwa sera ya uchumi wa buluu, idadi ya watalii Zanzibar imeongezeka na uchumi umeanza kukua.

Mwenyekiti huyo alisema uvuvi ni tegemeo kubwa litakalotoa ajira nyingi kwa vijana na kuongeza kipato kufanya shughuli zao za kimaendeleo na uti wa mgongo wa Wazanzibari ni uvuvi ndiyo maana azimio la Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Kwanza, ni kuboresha kilimo, ufugaji na uvuvi.

"Kilimo, ufugaji na uvuvi ni sekta za asili ambazo zinainua pato la taifa na ndiyo maana Mzee Karume aliboresha maeneo hayo na katika kipindi kifupi cha uongozi wake, Zanzibar iliendelea katika kuwekeza katika maendeleo," alisema.

Pia alisema endapo Wazanzibari watashirikiana na kuondoa tafauti zao za kisiasa, Zanzibar itapiga hatua kubwa kimaendeleo na Rais Dk. Mwinyi ana nia njema ya kukuza uchumi katika kuendeleza sekta ya uchumi wa buluu na uvuvi.

Naye Juma Kombo, mjumbe wa jumuiya hiyo, alisema vifungu vya 17 na 21 vya sheria hiyo endapo havitafanyiwa marekebisho, vitawasababishia matatizo makubwa baharini ikiwamo maafa, hivyo ni vyema serikali kuvitazama upya na kuvifanyia marekebisho kwa maslahi ya wavuvi na taifa.



Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, akimpongeza na kumkabidhi zawadi mmoja miongoni mwa wahitimu wa Chuo cha Afya cha Kwamchina Mwanza baada ya kumaliza mafunzo ngazi ya stashahada na astashahada, uwanja wa michezo wa Mao Dezong. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Waziri aweka wazi mpango kuendeleza wafanyabiashara

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

KAIMU Waziri wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na wafanyabiashara ili kufanikisha mikakati na mbinu za biashara kwa lengo la kuendeleza maendeleo ya sekta hiyo.

Akizungumza katika ufungaji wa tamasha la saba la biashara lilifonyika katika viwanja vya Maisara, Mjini Unguja, alisema uwapo wa matamasha ya biashara unawawezesha wafanyabiashara wa ndani na nje ya Zanzibar kubadilishana mbinu za biashara na kukuza soko la bidhaa hasa kwa wafanyabiashara wadogo ambao wanahitaji kukuza biashara zao.

Alisema Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itajitahidi kufanya kila linawozekana ili kuhakikisha tamasha linaendelea kufanyika kila mwaka na kutoa fursa mbalimbali za biashara ndani na nje ya Zanzibar.

"Matamasha haya pia yatawawezesha wafanyabiashara kupata masoko ili kuwawezesha wafanyabiashara kukuza mitaji yao na hatimaye kukuza uchumi wa Zanzibar.

"Tamasha hili limeleta faida kubwa, limetoa fursa nyingi kwa wafanyabiashara wetu hasa wadogo ambao wamejitangaza kibiashara na kupeana mbinu mbalimbali za biashara pamoja na kubadilishana uzoefu na limewawezesha wananchi wetu kupata bidhaa mbambali kwa bei nafuu," alisema waziri

Tamasha hilo, alisema limeweka historia nzuri kwa wafanyabiashara kutokana na mauzo kuwa juu pamoja na kuwa wengi. Alisema zaidi ya wajasiriamali 200 wameshiriki tamasha hilo na kuuza bidhaa zao kwa kiwango kikubwa.

Waziri huyo aliwataka wafanyabiashara kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali pamoja na kuzisajili biashara zao ili kutambulika na kuwa rasmi hatimaye kuondoa changamoto za biashara na kuiwezesha serikali kukusanya kodi kwa urahisi kwa maendeleo ya nchi.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Juma Reli, alisema malengo ya tamasha hilo yamefanikiwa kwa asilimia kubwa kutokana na soko na mauzo ya bidhaa kuwa juu, hivyo kusababisha baadhi ya wafanyabiashara kuuza bidhaa zote na kupata faida.

Alisema wizara bado inaendelea kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ambayo itakayozidi kuboresha tamasha hilo ikiwamo kuanzisha mashindano ya bidhaa, mafunzo ya ubunifu na mbinu za biashara ili kuzidisha ubora wa bidhaa na kulifanya lizidi kuwa bora na kuleta tija kwa wafanyabiashara, serikali na wananchi kwa ujumla.

Aidha, Katibu Mkuu huyo alisema tamasha hilo linatarajiwa kufanywa mara mbili kwa mwaka na kutaka lifanyike katika eneo la kudumu huko Nyamanzi Wilaya ya Magharibi "B" nje kidogo ya mjini Zanzibar.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, alisema serikali ya mkoa itahakikisha kuwapo ulinzi na usalama muda wote wa tamasha na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa wadau wote waliofanikisha kufanyika tamasha hilo.

# Rwanda yaagiza shule zote za umma zifungwe tena

**Kigali, RWANDA**

WIZARA ya Elimu Rwanda, imesema kuwa shule zote za umma na binafsi, chekechea, msingi na sekondari kufungwa kuanzia jana.

Hiyo ni husussan kwa mji wa Kigali kama njia moja ya kukabiliana na usambaaji wa virusi va corona.

Pia wanafunzi wa shule za bweni watasalia katika shule zao na wataendelea kupokea huduma muhimu.

Wizara hiyo pia iliongeza kuwa shule zote nje ya mji wa Kigali zitaendelea kufundisha na shughuli zingine za masomo kwa kuzingatia hatua kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19.

Pia mwongozo utapitiwa tena katika kipindi cha wiki mbili zijazo kulingana na tathmini ya huduma ya afya.

Watu 22 walikufa kutokana na Covid-19 kwa muda wa siku saba zilizopita na kuifanya idadi ya waliokufa kutokana na corona hadi kuifikia sasa kuwa 142.

Haya yanajiri wakati bado ikitekelezwa marufuku ya siku 15 ya usafiri wa umma kati ya wilaya na mji mkuu Kigali pia biashara zote nchini humo husitishwa saa 12 jioni.

BBC



Polisi na wanajeshi wakikabiliana na wahamiaji ili kuwalazimisha kurudi walikotoka. Takriban wahamiaji 7,000, wengi wao kutoka Honduras, wanakadiriwa kuwasili Guatemala tangu mwishoni mwa wiki. **PICHA/REUTERS**

# Maelfu ya wahamiaji wakwama kuingia Marekani

**Guatemala City, GUATEMALA**

MSAFARA wa wahamiaji kutoka Amerika Kusini uliokuwa ukielekea nchini Marekani, umekutana na marungu na gesi za kutoa machozi nchini Guatemala, huku vikosi vya usalama vikifunga njia ya kupita kuelekea Marekani.

Maelfu ya watu hao walizuiwa kwenye barabara karibu na mpaka wa Guatemala na Honduras.

Serikali ilisema haingekubali matembezi ya umati wa watu kinyume cha sheria.

Wahamiaji wanaokadiriwa kuwa 7,000, wengi wao kutoka Honduras, wameingia katika siku za hivi karibuni, wakikimbia umaskini na ghasia.

Wanatumaini kusafiri hadi Mexico na baadaye kuufikia mpaka wa Marekani.

Kila mwaka, maelfu ya wahamiaji wa Amerika ya kati hujaribu safari hii ili kujaribu kufika Marekani, mara nyingi hutembea kwa miguu.

Rais mteule wa Marekani, Joe Biden, kutoka Chama cha Democrat, ameapa kuondoa sera kali za uhamiaji zilizowekwa na mtangulizi wake, Donald Trump, kutoka Republican.

Utawala wa Biden, ambao utachukua mamlaka Jumatano, umewaonya wahamiaji kutofanya safari, kwa sababu sera za uhamiaji hazitabadilishwa haraka.

Wahamiaji wakivuka mpaka wa Guatemala kuelekea kwenye mpaka wake na Mexico, walizingirwa na vikosi vya usalama karibu na kijiji cha Vado Hondo kilichopo Kusini -Mashariki.

Kikundi cha wanajeshi na maofisa wa polisi walifunga barabara, na kuwazuia wengi wao kuendelea na safari.

Baadhi ya wahamiaji hao bado walilazimisha kwa nguvu kupita na kuwafanya maofisa wa usalama kuwasukuma nyuma.

Video iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, inaonyesha vikosi vya Guatemala vikitumia gesi za kutoa machozi, vifaa vya kujikinga na marungu kuwarudisha nyuma wahamiaji.

Watu kadhaa walijeruhiwa katika tukio hilo.

# Idadi ya waliofariki dunia Darfur sasa yafikia 80

**Dafur, SUDAN**

MADAKTARI nchini Sudan, wanasema zaidi ya watu 80 wameuawa katika kipindi cha siku mbili katika mapigano kati ya makabila mawili hasimu eneo la Darfur.

Mamia ya wengine wamejeruhiwa wakati wa mapigano hayo huko El Geneina.

Kambi iliyo karibu ya watu waliolazimika kutokwa, pia ilishambuliwa wakati wa mapigano hayo ambayo ndio mabaya kutokea tangu kufikiwa kwa makubaliano ya amani Oktoba mwaka jana.

Walinda amani wa kimataifa walianza kujiondoa Darfur kwa awamu kuanzia mapema mwezi huu.

Ripoti zinasema kuwa vurugu zilianza pale mwanaume mmoja wa Kiarabu alipochomwa kisu hadi kufa na mwanaume mwingine ambaye si mwarabu na kusababisha ufyatulianaji wa risasi.

Serikali ya Sudan inatuma vikosi vyake vyake katika eneo hilo kulinga raia.

**BBC**

# Wauawa wakishambuliwa na mtu asiyejulikana

**Kabul, AFGHANSTAN**

MAJAJI wawili wa kike wameripotiwa kupoteza maisha katika shambulizi la silaha kwenye gari katika mji mkuu wa Kabul, nchini Afghanistan.

Matukio Kama hayo yameendelea kutokea wakati wawakilishi kutoka miji kadhaa mjini Kabul na Taliban, wakikutana kuhusu amani mjini Qatar.

Idara ya polisi ya Kabul, ilitangaza kwamba majaji wa hao walishambuliwa saa mbili asubuhi na watu wasiojulikana kwenye eneo la Kale-i Fethullah katika mji mkuu.

Majaji hao kike walifariki dunia katika shambulizi hilo, na wengine wawili walijeruhiwa.

Hakuna mtu yeyote aliyedai kuhusika na shambulizi hadi kufikia sasa.

Rais wa nchi hiyo, alitoa taarifa kulaani shambulio hilo na kwa wananchi yakitekelezwa na Taliban na vikundi vingine vya kijeshi.

"Ugaidi si suluhisho la matatizo ya Afghanistan," alisema Rais huyo.

Kundi la Taliban limekanusha kuhusika na tukio hilo, ingawa lilisema wapiganaji wake wataendelea kufanya mashambulizi kwa viongozi mahsusi wa serikali.

**REUTERS/TRT**



# MESSI

## ALA KADI NYEKUNDU YA KWANZA BARCELONA

**SEVILLE, Hispania**

LIONEL Messi ameonyeshwa kadi yake ya kwanza nyekundu kwa kipindi alichoichezea Barcelona, wakati wakipoteza kwa Athletic Bilbao kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la Super Hispania.

Messi akicheza kwa mara ya 753 hapo Barca, alimpiga kwa nyuma Asier Villalibre katika sekunde za mwisho za muda wa nyongeza na tukio hilo lilinaswa na VAR.

Barca waliongoza mara mbili kupitia Antoine Griezmann, lakini Oscar de Marcos na Villalibre, waliisawazishia Athletic.

Na Inaki Williams akafunga la ushindi kwenye mchezo huo uliopigwa mjini Seville na kuonekana kuwa kwenye kumbukumbu ya kuwa wa burudani zaidi huku Athletic wakitwaa taji lao la pili tangu mwaka 1985, hadi tukio hilo lilipotokea.

Messi alimkwatua mfungaji Villalibre wakiwa hawana mpira katika dakika ya 120. Mwamuzi hakuliona tukio hilo hadi alipokwenda kutazama kwenye VAR na kumwonyesha kadi nyekundu Messi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ameonyeshwa kadi nyekundu mara mbili tu katika maisha yake ya soka, zote akiwa na Argentina - kwenye mchezo wake wa kwanza wa kimataifa dhidi ya Hungary mwaka 2005 na kwenye Copa America 2019 kutafuta nafasi ya tatu dhidi ya Chile.

Anaweza kufungiwa kwa mechi angalau nne baada ya kuonyeshwa kadi hiyo.

# DE BRUYNE AFIKISHA PASI ZA MWISHO 100

**MAMCHESTER, England**

KEVIN De Bruyne alitengeneza pasi ya mwisho ya 100 kwa Manchester City katika mashindano yote kwa kumtengea pande John Stones, aliyefunga bao la kwanza dhidi ya Crystal Palace.

Alifikisha idadi hiyo ya pasi za mwisho katika dakika ya 26 kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu England uliopigwa Jumapili.

Hiyo inamaana kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kwa sasa ametengeneza pasi za mwisho 31 kwenye Ligi Kuu England, zikiwa nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote tangu alipoanza kuichezea City mwaka 2015.

Katika pasi hizo za mwisho 100, alizozipiga kwenye Ligi Kuu ni 75 zikitokana na mechi 165, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, akiwa ametengeneza mabao 15 kwenye mechi 37 alizocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pasi za mwisho tano ametengeneza kwenye Kombe la FA, nne kwenye EFL - ambapo City imelibeba mara nne wakati De Bruyne akicheza hapo na moja kwenye mechi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# VIDAL: INTER IMETHIBITISHA UBORA KUIFUNGA JUVENTUS

**MILAN, Italia**

INTER Milan imethibitisha kwamba inaweza kutoa changamoto kubwa kwenye mbio za ubingwa msimu huu kwa kuwafunga mabingwa Juventus mabao 2-0, kwa mujibu wa Arturo Vidal.

Vidal alifunga bao la kwanza dhidi ya timu yake hiyo ya zamani pale kwenye dimba la San Siro, Jumapili, akiunganisha krosi ya Nicolo Barella na kuwa bao lake la kwanza kwenye Serie A tangu alipofunga wakati Juve wakibeba taji Mei 2015.

Alikuwa mchezaji wa kwanza wa zamani wa Juve kuifunga timu hiyo akiichezea Inter tangu Christian Vieri mwaka 2004.

Lautaro Martinez na Romelu Lukaku walikosa nafasi nzuri za kufunga ili kuipatia mabao zaidi Inter.

Nerazzurri hao ulikuwa ni ushindi wao wa kwanza kwenye ligi dhidi ya Juve tangu Septemba 2016 na ushindi huo ni mchezo wa kwanza kwao bila kuruhusu bao tangu Aprili 2010.

Kikosi hicho cha kocha Antonio Conte sasa kipo pointi sawa na vinara wa Serie A, Milan wakiwa na pointi 40. Milan walikuwa wanacheza jana Jumatatu na ushindi utawafanya waendelee kukaa kileleni.

"Ni muhimu kwangu mimi na kwa timu. Ulikuwa mchezo mgumu sana dhidi ya timu bora Italia," alisema Vidal akiiambia Sky Sport Italia.

"Najisikia fahari kufunga bao langu la kwanza kwa Inter, nina furaha sana. Nafikiri tumethibitisha kwamba tunaweza kupambana kwa ajili ya kuwania taji la Scudetto."



## HABARI MICHEZO



# DEPAY
## AZITAKA KLABU KUBWA TATU

**LYON, Ufaransa**

NYOTA wa Lyon, Memphis Depay, amesema yeye pamoja na mchezaji mwenzake klabuni hapo, Haussem Aouar, wanataka kucheza katika moja ya klabu bora tatu duniani.

Barcelona imekuwa ikimfuatilia kwa karibu mchezaji huyo, ambaye alihusishwa kutua katika Ligi ya LaLiga msimu ulioisha, lakini haikufanikiwa.

Mchezaji mwenza, Aouar pia alihusishwa kuihama klabu hiyo ya Ufaransa ambayo amehitimu hapo akademi ya vijana, huku Arsenal ikihusishwa naye.

"Tunajua tunataka kucheza katika klabu kubwa, lakini tunataka kwenda katika moja ya klabu kubwa tatu duniani," alisema Depay akiiambia Canal+.

"Hapo utamwona Houssem bora mara 10 zaidi, kwangu pia ni vivyo hivyo."

Mchezaji huyo pia amesema angetamani kushinda taji la Ligi Kuu Ufaransa akiwa na Aouar, timu pamoja na rais wa klabu hiyo.

# LEWANDOWSKI AWEKA REKODI MPYA BUNDESLIGA

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 21 katika kipindi cha kwanza cha msimu wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Gerd Muller hapo awali alikuwa akishikilia rekodi ya mabao 20 akiwa na Bayern ambayo aliiweka msimu wa 1968-69.

Lewandowski alifikia rekodi hiyo ya mabao 20 katika mchezo uliochezwa Januari 8, mwaka huu akifunga wakati Bayern ilipofungwa 3-2 na Borussia Monchengladbach.

Na juzi Jumapili, katika mchezo wa 16 wa Ligi ya Bundesliga yenye jumla ya mechi 34, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alimpita Muller kwa kuweka idadi hiyo ya mabao na kufikia 21.

Pia lilikuwa bao la tano la Lewandowski katika michezo yake minne iliyopita dhidi ya Freiburg.

Kuelekea mchezo wa Jumapili kwenye Uwanja wa Allianz, timu hiyo ya Bavaria ilikuwa na alama 33 kwa mara ya mwisho kuwa na alama nyingi baada ya mechi 15 ilikuwa ni msimu wa 2017-18.

Lewandowksi alifunga mabao 34 kwenye ligi msimu uliopita, tofauti ya mabao sita ya rekodi ya Muller ya Bundesliga ya mabao 40 (1971-72), lakini nyota huyo wa Poland sasa anaonekana vizuri kwenye harakati ya kuifukuzia idadi hiyo.





# OZIL ATUA RASMI FENERBAHCE

**LONDON, England**

MESUT Ozil ametua nchini Uturuki tayari kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kujiunga na klabu ya Fenerbahce, kwa mujibu wa Sky Sport.

Ozil anaondoka Arsenal Jumapili akiwa na rekodi ya kuwa mchezaji aliyekuwa akipokea mshahara mrefu zaidi kuliko wachezaji wengine (pauni 325,000 kwa wiki) licha ya kutokuwapo kwenye orodha ya wachezaji watakaoitumikia timu hiyo msimu huu.

Ozil aliagana na wachezaji wenzake kule Emirates muda mfupi baada ya kuruhusiwa kwenda Uturuki akaendelee na utaratibu wa kukamilisha usajili.

Klabu ya Fenerbahce ilithibitisha mchakato wa usajili wa Ozil unaendelea na hivyo iliwataarifu wawekezaji sambamba na soko la hisa la nchi hiyo juu ya kuanza kwa mazungumzo hayo.

Akifanya mahojiano mafupi kwa njia ya simu, Ozil aliambia NTV (ya Uturuki) "mimi ni shabiki wa Fenerbahce na ndio maana ninafurahi kuja Uturuki kuitumikia Fenerbahce. Mungu amenipa nafasi ya kuivaa jezi ya Fenerbahce kama shabiki.

"Mungu akipenda nitaivaa na kuitumikia kwa heshima kubwa kwa kila nitakachoweza kukifanya.

"Ni kweli sijacheza kwa muda sasa lakini nipo vizuri, sina tatizo lolote."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: SABABU SARE NA LIVERPOOL

●●●Tulijaribu kufunga na tukashindwa, kiwango kilikuwa bora na ilitosha sisi kushinda, lakini...

**LIVERPOOL, England**

MANCHESTER United "ilikosa nafasi" ya kuifunga Liverpool, amesema kocha Ole Gunnar Solskjaer baada ya kikosi chake kubakia kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England kwa sare ya bila kufungana na Liverpool.

Ulikuwa mchezo wenye matarajio makubwa kwa timu zote mbili na Solskjaer anajua kwamba, kikosi chake kilikuwa bora zaidi ya wapinzani wao na kudai walitakiwa kupata ushindi pale kwenye dimba la Anfield.

Liverpool, ikiwa bila ya walinzi wake wa kati muhimu na nafasi ya beki wakicheza viungo Jordan Henderson na Fabinho, walitawala kipindi cha kwanza, lakini walikuwa United ambao walikaribia kufunga wakati mpira wa adhabu ndogo wa Bruno Fernandes wa umbali wa yadi 20 kupaa nje kidogo ya goli.

Fernandes tena alimjaribu golikipa wa Liverpool, Alisson kabla ya shuti la Thiago kuokolewa na David de Gea.

Alisson alikuwa shujaa wa Liverpool wakati alipookoa vizuri mpira wa Paul Pogba.

"Ilikuwa ni nafasi nzuri tuliyoikosa, lakini kwa mara nyingine tena tulikuwa tunacheza na timu nzuri zaidi," alisema Solskjaer akiiambia BBC Sport.

"Nimekatishwa tamaa, lakini pointi moja bado ni muhimu kama tutashinda mchezo unaofuata.

"Tumeimarika na kuwa kwenye kiwango bora kabisa. Ni matokeo tu ndio yametukatisha tamaa, lakini kiwango kilikuwa kizuri. Najua vijana hawa wanaweza kucheza vizuri zaidi."

United sasa inaongoza kileleni mwa msimamo kwa pointi mbili wakifuatiwa na Manchester City, ambao wamejivuta nafasi ya pili baada ya kuifunga Crystal Palace mabao 4-0, na Leicester City wapo nafasi ya tatu.

Liverpool, ambao wamefunga bao moja tu katika mechi zake nne kwenye mechi nne za ligi zilizopita, wamevutwa hadi nafasi ya nne.

"Nafikiri kiwango kilikuwa bora na ilitosha sisi kushinda, lakini kushinda mchezo unatakiwa kufunga mabao na hatukufanya hivyo, ndio maana tulipata matokeo yale," alisema Klopp.

"Tulijaribu kufunga na tukashindwa kufunga."

## KWA UFUPI

### DILI LA DELE BADO GUMU
KIUNGO wa Tottenham Hotspur na England, Dele Alli, mwenye umri wa miaka 24, "anataka" kuhamia kwa mabingwa wa Ufaransa, Paris St-Germain, lakini mazungumzo baina ya timu hizo yamekuwa magumu. ***(Mwandishi Fabrizio Romano, kupitia Twitter)***

### WEST HAM KUMSAJILI LABORDE
KLABU ya West Ham United inapima uwezekano wa kumsajili mshambuliaji kutoka Ufaransa, Gaetan Laborde mwenye umri wa miaka 26, ambaye kwa sasa anachezea klabu ya Montpellier. ***(Telegraph)***

### GRACIA ATAKIWA BARCA
MAKAMU wa Rais wa Barcelona, Carles Tusquets, amependekeza kumsajili mlinzi wa Manchester City na Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 20, kwa euro milioni nane kwa wagombea watatu wa urais wa klabu hiyo, lakini hakuna kinachoweza kufanyika kwa sasa, hadi baada ya uchaguzi mkuu Machi. ***(Marca)***

### DEPAY ATAKA KLABU KUBWA
MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 26, amesema yeye na mchezaji mwenzake wa klabu ya Lyon, Houssem Aouar mwenye miaka 22, wanataka kuhamia katika "moja ya klabu tatu kubwa duniani." Depay amekuwa akihusishwa na klabu ya Barcelona, huku kiungo kutoka Ufaransa Aouar akiripotiwa kunyemelewa na Arsenal. ***(Canal+)***

### BALE ATANG'ARA TENA
NAHODHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Michael Dawson anaamini ni suala la muda tu kabla Gareth Bale kuonyeshwa kiwango chake cha juu zaidi.

### FULHAM KUSAJILI MAPEMA
KOCHA wa Fulham, Scott Parker amesema anataka kusajili wachezaji na kumaliza biashara ya usajili mapema katika dirisha la mwezi huu. ***(Evening Standard)***

### SANSON AWANIWA EPL
KOCHA wa Marseille, Andre Villas-Boas, amethibitisha kuwa kiungo wa Ufaransa, Morgan Sanson mwenye umri wa miaka 26, ananyemelewa na klabu kadhaa za England zikiwamo Arsenal, Aston Villa, Tottenham na West Ham. ***(Mail)***

### INTER KUTOSAJILI JANUARI
MKURUGENZI wa soka wa Inter Milan, Beppe Marotta, amesema kuwa klabu hiyo ipo vizuri kifedha, lakini haitafanya uwekezaji wowote wa wachezaji katika dirisha la usajili la mwezi huu. ***(Sky Sport Italia)***

### ERIKSEN KURUDI SPURS
KUNA uwezekano mkubwa kwa Christian Eriksen kurudi katika klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur Januari hii. Nyota huyo wa kimataifa wa Sweden mwenye umri wa miaka 28, ameshindwa kupata namba ya kudumu pale Inter Milan.

### LEWSI-POTTER HAUZWI
KOCHA wa Hull City, Grant McCann, ametangaza kuwa mshambuliaji kinda wa klabu hiyo, Keane Lewis-Potter mwenye umri wa miaka 19, hauzwi, ingawa mazungumzo juu ya mkataba mpya baina ya Hull na mchezaji huyo yanaelekea kugongo mwamba. ***(Yorkshire Post)***

### MILAN WAKARIBIA KWA TOMORI
KLABU ya AC Milan inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mlinzi wa kati wa Chelsea, Fikayo Tomori kwa mkopo, huku kukiwa na uwezekano wa kumsajili moja kwa moja kwa pauni milioni 25.

# BIGIRIMANA CHANZO LUSAJO KUREJESHWA NAMUNGO FC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Numungo umesema uamuzi wa kumrejesha kikosini aliyekuwa mshambuliaji wao, Lusajo Relliants, ni ili kuchukuwa nafasi ya Blaise Bigirimana ambaye kwa sasa ni majeruhi.

Lusajo aliachana na miamba hiyo ya Ruangwa mkoani Lindi baada ya kumalizika kwa msimu uliopita na kwenda kujiunga na timu ya Polisi Tanzania yenye maskani yake mkoani Kilimanjaro, lakini sasa amerejea Namungo kupitia usajili wa dirisha dogo lililofungwa Ijumaa iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Suleiman, alisema usajili wa Lusajo umekuja baada ya Blaise kuvunjika mguu katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Simba iliyopigwa Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar, ambapo sasa atatakiwa kukaa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi sita.

Alisema ulifikia uamuzi huo baada ya mapendekezo ya Kocha Mkuu, Hemed Morocco, kuhitaji mshambuliaji ambaye ataziba nafasi iliyoachwa wazi na Blaise baada ya kuumia.

"Blaise, leo (jana), alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Muhimbili Kitengo cha MOI kwa ajili ya matibabu na kutakiwa kukaa nje ya uwanja kwa muda wa miezi sita. "Uongozi tumejiuliza ni mshambuliaji gani anafaa, tumeona Lusajo ambaye amekuja kwetu na kutueleza kwamba yupo tayari kuitumikia tena timu yetu, tukaamua kumpa mkataba wa miaka miwili," alisema Suleiman.

Alisema katika usajili wao mwingine, wamempa mkataba wa miaka miwili, Erick Kwizera, kutoka Burundi na Ibrahim Abdallah anayecheza nafasi ya kiungo kutoka Malindi ya visiwani Zanzibar.

Katibu huyo alisema kulingana na mashindano yaliyopo mbele yao ikiwamo Kombe la Shirikisho Afrika, Ligi Kuu Bara na FA, wamelazimika kuboresha kikosi chao katika safu ya ushambuliaji na kiungo.

Aidha, katibu huyo amewataja nyota watatu wakiwamo wawili walioachana nao ambao ni Edward Manyama aliyemaliza mkataba na kujiunga na Ruvu Shooting na Mghana Joseph Kwasa huku Zakari Mkumbo wakimpeleka kwa mkopo Geita FC.

# DStv sasa yaja na Promosheni kali ya 'Panda Tukupandishe'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania, imetangaza promosheni maalum kwa wateja wa DStv ijulikanayo kama 'Panda Tukupandishe' ambapo kwa kipindi cha miezi mitatu itakuwa ikiwapandisha vifurushi wateja wake.

Hii ni promosheni inayowawezesha wateja wa DStv wanaokidhi vigezo (wateja ambao akaunti zao zimekatika, wateja wanaoendelea na wateja wapya) kupata fursa ya kulipia kifurushi kinachofuatia cha juu yake na kupandishwa kwa kupatiwa kifurushi cha juu ya kile alicholipia kwa muda maalum ambapo itategemea na kifurushi ambacho mteja alikuwa amelipia hadi kufikia Januari 8, mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, alisema pia itatumika kwa kifurushi mteja alichojiunga nacho baada ya Janurai 8.

"Tunafurahi kuzindua rasmi promosheni maalum ya 'Panda Tukupandishe' hii ikiwa ni njia mojawapo ya kuwashukuru wateja wetu kwa kuendelea kuwa nasi na pia njia ya kuwahakikishia kuwa tumejipanga vema kuendelea kuwapatia burudani isiyo na kifani.

"Promosheni hii iko namna hii, mfano mteja wa kifurushi cha Bomba, akilipia kifurushi cha Family, atapandishwa hadi kifurushi cha Compact bila malipo ya ziada kwa mwezi mmoja," amesema Shelukindo.

Alisema kampuni hiyo inaendelea kuwapa wateja wake burudani ya kina bila kusahau maudhui mengine kama babari na elimu, huku ikihakikisha kuwa wateja wake wanapata maudhui kemkem na ya kusisimua ya ndani na nje.

Kaimu Meneja wa Thamani kwa Wateja, Lucy Kisasa, akitolea ufafanuzi wa promosheni hiyo, alisema kama zilivyo nyingine, kuna vigezo na masharti ambavyo vitafuatwa ili mteja aweze kunufaika ambapo kwanza kabisa ni kwa wateja wa DStv waliopo Tanzania, wale ambao akaunti zao ziko hai na kwa wale akaunti zao zimekatika huku pia ikiwahusu wateja wapya wa wanaojiunga sasa na huduma hizo.

Alisema kwa wateja wa DStv ambao wamelipia kifurushi chao kwa mwaka mzima hawahusiki na promosheni hii kwa kuwa wao tayari wana ofa yao ambapo hupata mwezi mmoja wa kifurushi chao bila malipo ya ziada.

Akifafanua zaidi, Lucy alisema mteja atakayetaka kulipia kifurushi cha juu yake kabla ya kifurushi alichonacho kumalizika naye atanufaika na ofa hiyo na pia salio lake la kifurushi cha awali kitaendelea kubaki kwenye akaunti yake na hivyo kuweza kulitumia tena punde ofa aliyopata itakapokamilika kulingana na vigezo na masharti.

TUNAWAPANDISHA...



Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa Promosheni ya 'Panda Tukupandishe' maalum kwa ajili ya wateja wa DStv, iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Klabu Ligi Kuu Z'bar zamng'oa m/kiti bodi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VIONGOZI wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar wamepiga kura ya kutokuwa na imani na Mwenyekiti wa Bodi ya ligi hiyo, Kassim Mohmed.

Jumla ya viongozi wa klabu tisa waliohudhuria mkutano huo walioitisha juzi, walipiga kura ya hapana ya kumkataa mwenyekiti huyo wa bodi kwa kile walichokieleza kuwa ni kuvujisha siri za vikao vya klabu na kuzipeleka kwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF). Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wajumbe wa Bodi ya Ligi, Mohammed Massoud, alisema wanaheshimu uamuzi ya viongozi hao wa klabu kwa kuwa wao ndio waliowachagua kuwapo katika bodi hiyo ya ligi.

Alisema awali walifanya vikao vya mara kwa mara ili kuunusuru msuguano uliopo baina ya klabu na mwenyekiti wa bodi hiyo, lakini jitihada hizo hazikufanikiwa mpaka kufikia hatua ya klabu kumwondosha kwa kumpigia kura ya kutokuwa na imani naye.

"Tulijaribu kukaa na klabu na mwenyekiti kumuita kuangalia kuna tatizo gani, lakini hatukufikia muafaka, hii inaonyesha klabu haziko tayari kufanya kazi na mwenyekiti wa bodi ya ligi kutokana na madai yao mbalimbali," alisema huku akifafanua kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Sheha Momhed atafanya kazi za mwenyekiti hadi hapo atakapopatikana mwingine.

## Usajili waipa jeuri Yanga Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema usajili ambao umefanywa katika safu yao ya ushambuliaji, sasa unawapa jeuri ya kutamka kwamba, hakuna timu itakayowazuia kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwambusi alisema msimu huu wako vizuri na wana imani kwa mwenendo wa timu yao hakuna itakayowasumbua.

Alisema malengo yao makubwa msimu huu ni kufanya vizuri kila mechi iliyopo mbele yao na kwamba baada ya kutwaa Kombe la Mapinduzi sasa wako imara zaidi kwa ajili ya Ligi Kuu.

"Tumefanya usajili wa wachezaji watatu, Saidi Ntibazonkiza ambaye tayari ameonekana makali yake, lakini pia kuna Dickson Job na tumefunga dirisha kwa kuimarisha safu ya ushambuliaji kwa Fiston Abdul Razak.

"Tumeongeza watu ambao wanaleta ushindani na kuimarisha kikosi, ninaimani tutakaporejea kutoka mapumziko tunaendelea tulipoishia ni kutafuta pointi tatu kila mechi," alisema Mwambusi.

Naye Meneja wa timu hiyo, Hafidhi Salehe, alisema baada ya kurejea kutoka visiwani Zanzibar wachezaji wamepewa mapumziko ya siku 10 na baada ya hapo wote watarejea kambini kuendelea na maandalizi ya mzunguko wa pili.

**Michezo**

Jumanne Januari 19, 2021

Nipashe



SOLSKJAER: SABABU SARE NA LIVERPOOL HABARI UK 22

CHINI YA ULINZI...



Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane, akipata ushindani mkali kutoka kwa safu ya ulinzi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

# FISTON AANIKA MKATABA YANGA, AJIWEKA SOKONI

## ●●● Asema ana miezi sita ya kuichezea Yanga, ni kama ilivyokuwa kwa Morrison, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, kueleza kuwa usajili wao mpya, Mrundi Fiston Abdul Razak, aliyesajiliwa katika dirisha hili dogo ni moto wa kuotea mbali mbele ya goli huku akimudu vema kutengeneza nafasi, straika huyo amejiweka sokoni baada ya kuanika mkataba wake ambao ni wa muda mfupi ndani ya mabingwa hao wa Kombe la Mapinduzi.

Kwa muda mrefu, Kaze amekuwa akilalamika safu yake ya ushambuliaji kukosa umakini mbele ya lango kwa kushindwa kuzibadili nafasi wanazozitengeneza kuwa mabao, jambo ambalo aliahidi kulifanyia kazi katika dirisha dogo lililofungwa Ijumaa iliyopita, ambapo klabu hiyo ilimsajili Fiston ambaye ni pendekezo la kocha huyo.

Awali akimzungumzia Fiston, Kaze alisema ni mchezaji mzuri anayejua kufunga akicheza nyuma ya mshambuliaji ama kama winga, na kwamba anaamini atakuwa msaada mkubwa katika safu yake ya ushambuliaji.

Kaze anaamini Fiston anaweza kuwa msaada mkubwa katika kikosi hicho akisaidiana na Mrundi mwenzake, Saidi Ntibazonkiza, ambaye naye amesajiliwa katika dirisha hili dogo na tayari ameshaonyesha uwezo mkubwa katika safu ya ushambuliaji ya timu hiyo ambayo hadi sasa imecheka na nyavu mara 29 kwenye mechi 18 za Ligi Kuu Bara. Lakini ni wazi, Fiston amejiweka sokoni baada ya kueleza kuwa kwa sasa amesaini mkataba wa miezi sita tu, na pengine anaweza kuongeza baada ya hapo.

"Nafurahi kujiunga na Yanga, ni timu kubwa na yenye historia kubwa, sasa nimetimiza malengo yangu ya kuichezea timu hii.

"Tulipokuja (na timu ya Taifa ya Burundi) kucheza dhidi ya Taifa Stars, kuna kiongozi mmoja alikuja hotelini kwetu akaniambia unaonaje kama utajiunga na Yanga, nikamwahidi ipo siku moja, hivyo leo ninafurahi nimetimiza ahadi yangu. "Nimejiunga na klabu hii kwa miezi sita, labda baada ya hapo naweza kuendelea zaidi," alisema Fiston ambaye Yanga inakuwa klabu yake ya 11 kuichezea tangu aanze kucheza soka la ushindani.

Kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), mchezaji mwenye mkataba wa miezi sita, anaruhusiwa kuanza kufanya mazungumzo na klabu nyingine, hivyo Fiston yupo huru kuanza kufanya hivyo endapo atahitaji.

Fiston si mchezaji wa kwanza kusajiliwa na Yanga katika dirisha dogo na kupewa kwanza mkataba wa miezi sita, kwani msimu uliopita kwenye dirisha dogo klabu hiyo ilifanya hivyo kwa winga Mghana Bernard Morrison, ambaye baada ya kumaliza akajiunga na Simba kwa mvutano mkubwa na klabu yake ya awali.

Hadi sasa, Yanga inavutana na Morrison na imekata rufani Mahakama ya Usuluhishi ya Masuala ya Soka (CAS), ikipinga hukumu iliyotolewa na Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), ambayo ilimpa ushindi mchezaji huyo kwa kumtangaza yupo huru, hivyo kujiunga na Simba.

# STARS, ZAMBIA MECHI YA KIBABE CHAN LEO

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema kikosi chake kipo tayari kwa mechi ya leo ya michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Zambia, wakati timu hizo zitakaposhuka dimbani kwenye mechi yao ya Kundi A itakayopigwa majira saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Stars na Zambia zitashuka katika Uwanja wa Limbe/Buea nchini Cameroon leo, kila moja ikitaka kutangaza ubabe dhidi ya mwenzake na kuweka rekodi ya ushindi baada ya timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya Kundi A ya michuano hiyo mwaka 2009 nchini Ivory Coast.

Hii ni mara ya pili kwa timu hizo kupangwa kundi moja wakati huu zikiwa Kundi D pamoja na Guinea na Namibia, lakini mwaka 2009, zilipangwa Kundi A pamoja na Senegal na Ivory Coast, na zilipokutana zilitoka sare ya bao 1-1 la Tanzania likifungwa na Shadrack Nsajigwa.

Akizungumzia kikosi chake, Ndayiragije alisema maandalizi kwa ajili ya mechi hiyo yamekamilika na kilichobaki ni kila mmoja kuiombea Taifa Stars ifanye vizuri kwenye mechi hiyo ambayo anaamini itakuwa ngumu kwa kila upande lakini akieleza kuwa wamejipanga kupata matokeo.

Alisema wachezaji wake wana morali wa kufanya vizuri na tayari Erasto Nyoni ambaye alibaki nchini kutokana na matatizo ya kifamilia, amejiunga na wenzake kambini baada ya kuwasili Cameroon tangu juzi.

Michuano hiyo ambayo ilianza rasmi Jumamosi iliyopita, imepangwa katika makundi manne kila moja likiwa na timu nne na timu mbili zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili kutoka kila kundi zitatinga hatua ya robo fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042